Kiswahili

Kiongozi cha Mwalimu
Darasa la Sita



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI

NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 232

Jina la Chapisho: Kiswahili Kiongozi cha Mwalimu Darasa la Sita

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-050-1

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 22 Septemba, 2019 kuwa Kiongozi cha Mwalimu kwa ajili ya Darasa la Sita katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Kitabu cha Mwanafunzi cha Kiswahili Darasa la Sita, 2019.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kaimu Kamishna wa Elimu.

Taasisi ya Elimu Tanzania

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 1 26/07/2021 12:02

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978-9987-09-050-1

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P. 35094

Dar es Salaam - Tanzania

Simu: + 255 735 041 170/ + 255 735 041 168

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutokaTaasisi ya Elimu Tanzania.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 2 26/07/2021 12:02

Yaliyomo

Ukurasa

Utangulizi.....**v**

Shukurani.....**xii**

Sura ya Kwanza

Kuimba wimbo wa kizalendo.....**1**

Sura ya Pili

Shairi.....**9**

Sura ya Tatu

Igizo la elimu ya biashara.....**21**

Sura ya Nne

Hadithi.....**27**

Sura ya Tano

Taswira za nahau.....**34**

Sura ya Sita

Ziara.....**45**

Sura ya Saba

Mawasiliano ya simu.....**55**

Sura ya Nane

Aina za maneno.....**65**

Sura ya Tisa

Risala.....**75**

Sura ya Kumi

Kutumia kamusi.....**82**

Sura ya Kumi na Moja

Matangazo ya biashara.....**90**

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 3 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Mbili
Uundaji wa maneno.....**99**
Sura ya Kumi na Tatu
Ufupisho.....**106**
Sura ya Kumi na Nne
Kumbukumbu za mikutano.....**112**
Sura ya Kumi na Tano
Umiliki katika lugha.....**120**
Sura ya Kumi na Sita
Kuandika habari.....**128**
Sura ya Kumi na Saba
Shairi la mabadiliko ya hali ya hewa.....**134**
Sura ya Kumi na Nane
Kusikiliza habari ya madhara ya rushwa.....**142**
Sura ya Kumi na Tisa
Kubaini hoja katika majadiliano.....**150**
Sura ya Ishirini
Kusoma kwa ufasaha.....**157**
Sura ya Ishirini na Moja
Kusoma kwa burudani.....**165**

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 4 26/07/2021 12:02

Utangulizi

Kitabu hiki cha Kiongozi cha Mwalimu ni cha nne katika mfululizo wa vitabu vitano vya kiongozi kwa somo la Kiswahili kuanzia Darasa la Tatu mpaka Darasa la Saba kilichoandaliwa mahususi kufundishia wanafunzi wa Darasa la Sita. Lengo kuu la kiongozi hiki ni kukupa mbinu na maarifa ya kufundisha somo la Kiswahili katika Darasa la Sita. Katika kiwango hiki, mwanafunzi anatakiwa aweze kumudu vizuri stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika Kiswahili katika miktadha mbalimbali.

Lugha iliyotumika katika matini, msamiati, miundo, mazoezi ya lugha, methali, nahau na vitendawili ni ya kiwango cha juu kuliko ya Darasa la Tano. Mbinu mbalimbali za ufundishaji zimependekezwa. Una uhuru wa kubuni mbinu zingine kulingana na mazingira, hali ya mahali, idadi na uwezo wa wanafunzi wako ili kuleta ufanisi katika ujifunzaji. Katika mchakato wote wa ufundishaji na ujifunzaji, washirikishe wanafunzi katika mazungumzo, kuimba, kuchora, kuigiza, kutamba na kughani.

Vifuatavyo ni vipengele muhimu ambavyo vitakusaidia kufundisha stadi za lugha katika Darasa la Sita.

1. Msamiati

Ni jambo muhimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wanafahamu maneno yote mapya na kuyatumia katika sentensi. Msamiati ufundishwe kwa kutumia vitu halisi, picha, vielelezo, maelezo, vitendo, maigizo na maonesho. Kwa hiyo, huna budi kutayarisha zana za kutosha za kufundishia na kujifunzia hasa zinazopatikana katika mazingira yako. Vidokezo vifuatavyo ni muhimu:

(a) Kutumia vitu halisi

Ni muhimu utumie vitu halisi katika kufundisha msamiati kwa kuwa, wanafunzi wanapoona, wanaelewa kwa urahisi.

(b) Kutumia picha na vielelezo mbalimbali

Iwapo utashindwa kupata vitu halisi, tumia picha na

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 5 26/07/2021 12:02

vielelezo. Picha na vielelezo vitayarishwe mapema na viwe vikubwa vya kutosha ili viweze kuonekana kwa urahisi kwa wanafunzi wote. Viwe na mvuto na uhalisia ili kueleza dhana kwa usahihi. Zingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Kwa mfano, tumia picha kubwa na vielelezo mguso ili kuwasaidia wanafunzi wenye uoni hafifu au wasioona, mtawalia.

(c) Kutumia vitendo

Inafaa maneno mengine, hasa vitenzi na vivumishi, yafundishwe kwa vitendo. Kwa mfano, chagua mwanafunzi na kumpa kifutio na kumwelekeza aende kufuta ubao. Mwanafunzi atafanya kama alivyoelekezwa. Akishamaliza, uliza swali. _____ (*Taja jina la mwanafunzi*) alikuwa anafanya nini? Pokea majibu na kisha eleza kuwa unafundisha neno "futa".

2. Miundo

Muundo ni mpangilio wa maneno na uhusiano wake katika sentensi. Katika muundo mmoja, inawezekana kutunga sentensi kadhaa zenye maana tofauti.

Katika kitabu cha mwanafunzi alama za kistari (yaani ____) na dotidoti (yaani…) zinatumika kuonesha nafasi ya kujaza miundo iliyolengwa. Alama ya kistari huonesha kuwa neno halijakamilika. Alama ya dotidoti huonesha kuwa neno au maneno hayapo. Katika miundo, nafasi hizo zinatakiwa zijazwe. Nafasi ya kistari itajazwa na sehemu ya neno na dotidoti itajazwa kwa neno au maneno. Waongoze wanafunzi kujaza nafasi hizo. Kwa mfano:

(a) Muundo "ana____" unaweza kujazwa na kuwa:
ana<u>lima</u>, ana<u>soma</u>, ana<u>imba</u>, ana<u>tembea</u> na kuendelea.

(b) Muundo "….. ata__" unaweza kujazwa ukawa *<u>Bibi</u> ata<u>kuja</u>.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 6 26/07/2021 12:02

Miundo ifundishwe kwa lugha rahisi na inayoeleweka. Irudiwerudiwe ili wanafunzi waizoee na kujenga kumbukumbu. Sentensi zinazotungwa kusisitiza miundo lazima zilingane na mazingira na maisha ya wanafunzi ili waweze kuzitumia katika maisha yao ya kila siku. Andaa mazoezi ya ziada kutokana na misingi ya sura husika.

3. Methali

Methali zifundishwe kadiri zinavyotokea katika hadithi au zijengewe maelezo yanayohusiana na mazingira zinamotumika. Eleza methali kwa kutumia masimulizi yanayohusiana na maisha ya kila siku. Ili wanafunzi wagundue maana za methali hizo, unaweza kufundisha methali zinazofanana au zisizo fanana na zile zilizomo katika hadithi. Ufundishaji wa methali bila kuzihusisha na mazingira ya maisha haufai. Wanafunzi waelekezwe kutoa mianzo au miisho ya methali zao na wengine wamalizie. Pia, wanafunzi waongozwe kutumia methali katika miktadha mbalimbali.

4. Vitendawili

Fundisha vitendawili kwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kutega na kutegua vitendawili vyao. Waelekeze kupeana mji kila wanaposhindwa kupata jibu sahihi. Uhusiano uliopo kati ya kitendawili na jibu lake ujadiliwe. Vitendawili pia vinaweza kutumiwa kama chemshabongo mwanzoni mwa somo la Kiswahili. Vitendawili vipya vyenye mantiki vikubaliwe. Kumbuka kwamba vitendawili hutofautiana kulingana na mazingira.

5. Misemo na nahau

Fundisha misemo na nahau kwa maelezo, picha, matendo, vitu halisi na majadiliano. Waongoze wanafunzi jinsi ya kutumia misemo na nahau hizo katika sentensi. Kwa mfano, maneno yako yalimkata maini ikiwa na maana ya *maneno yako yalimuudhi kupindukia*.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 7 26/07/2021 12:02

6. Ufahamu

Lengo la kusoma ni kuelewa kilichoandikwa, yaani ufahamu. Kuna njia mbalimbali za kufundishia kusoma. Unashauriwa kufuata mwongozo uliotolewa katika kitabu hiki. Hata hivyo, uwe huru kubadili njia iwapo utapata vikwazo kwani ufanisi wa mwanafunzi ndilo lengo letu. Zifuatazo ni njia mbalimbali za kusoma:

(a) **Kusoma kimya**

Katika somo la kusoma kimya, waelekeze wanafunzi kusoma kimya bila kufungua mdomo. Wanafunzi wasome sura yote na kujibu maswali ya ufahamu. Licha ya maswali yaliyomo kitabuni, tunga maswali mengine ya nyongeza kuhusiana na sura husika.

(b) **Kusoma kwa sauti**

Lengo la kusoma kwa sauti ni kuwawezesha wanafunzi kusoma kwa lafudhi sahihi ya Kiswahili kwa kuzingatia sauti ya kutosha, matamshi, shadda, kiimbo, matumizi ya alama za uandishi kwa usahihi na hisia. Katika somo la kusoma kwa sauti, onesha mfano wa usomaji mzuri. Pia, teua wanafunzi wengi kadiri iwezekanavyo wasome kwa sauti. Hii itategemea muda, idadi na kiwango cha usomaji wa wanafunzi.

(c) **Kusoma kwa ziada**

Lengo la kusoma kwa ziada ni kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa ufahamu, kasi stahiki na kumwongezea maarifa. Kusoma kwa ziada pia humjengea mwanafunzi tabia ya kupenda kujisomea. Ongoza usomaji huu. Yafuatayo yazingatiwe kutekeleza jambo hili:

(i) Waelekeze sura ya kusoma katika kipindi hicho;

(ii) Wanafunzi wasome kimya;

(iii) Waulize maswali. Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kuzungumza au kwa kuandika. Waongoze wanafunzi kutoa muhtasari wa habari waliyoisoma;

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 8 26/07/2021 12:02

(iv) Katika baadhi ya vipindi, badala ya kujibu maswali, wanafunzi waelekezwe kuchora, kusimulia, kuigiza au kuimba ili kukazia maarifa waliyoyapata; na

(v) Inafaa somo la kusoma kwa ziada lifanyike mara moja ndani ya wiki mbili.

7. Mazoezi ya lugha

Katika kitabu hiki, yamo mazoezi mbalimbali ya lugha kwa kila sura. Mazoezi hayo yamejumuisha uchaguzi wa jibu sahihi, kujaza nafasi, kueleza maana za maneno, kuunganisha sehemu mbili za sentensi au zaidi, umoja na wingi, kubadili nyakati na mengineyo. Fundisha zoezi moja au mawili ya lugha kwa kipindi kimoja na kuongeza mazoezi kulingana na mazingira na uwezo wa wanafunzi.

8. Utungaji

Sehemu kubwa ya mazoezi ya utungaji katika darasa hili ni wa kuongozwa. Uongozi huo unafanywa kwa:

(a) Kuchagua na kupanga sentensi zilizochanganyika, hasa zilizotokana na habari iliyosomwa au kuzungumzwa;

(b) Kutumia picha. Wanafunzi wanaweza kuchora, kama wataelekezwa na mwalimu kufanya hivyo. Wanaweza pia kuchorewa picha zinazohusu habari fulani. Wanafunzi wanatakiwa kutoa maelezo kuhusu picha moja au zaidi zilizotolewa;

(c) Kukamilisha habari;

(d) Kusimulia na kuelezea hadithi au habari mbalimbali. Wanafunzi wahimizwe kuigiza, kuimba, kutenda na kuitikia; na

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 9 26/07/2021 12:02

(e) Kuuliza maswali ambayo majibu yake yataunda hadithi.

Toa uzito sawa wa mazoezi ya utungaji wa mdomo na wa kuandika. Hii itawasaidia wanafunzi kukuza uwezo wa kujieleza kwa mdomo na kwa maandishi.

9. Ushairi

Ushairi ni uwanja mwingine wa fasihi. Katika kiwango hiki, mwanafunzi asome na kuimba mashairi na ngonjera. Pia, atambue vina, mizani, mishororo na urari katika mashairi. Vilevile, aelewe mawazo makuu na ujumbe uliomo katika shairi.

10. Mwandiko

Kazi ya kufundisha mwandiko iliyoanza Darasa la Kwanza, iendelezwe na kuimarishwa katika darasa hili. Sisitiza uumbaji mzuri wa herufi, hati ya kuunga, ukataji wa maneno kwa kuzingatia silabi na nafasi kati ya neno na neno. Pia, alama za uandishi zisisitizwe. Sisitiza usahihi wa mwandiko katika kila somo linalohusisha kuandika.

11. Imla

Ni somo ambalo mwanafunzi hupimwa uwezo wa kusikiliza na kuandika kwa usahihi kile walichosomewa na mwalimu. Wanafunzi wengi hawawezi kuandika habari vizuri kwa kufuata taratibu na alama za uandishi. Vilevile, hawawezi kuandika kwa kasi kwa kufuata msomaji anavyosoma. Fundisha uandishi wa imla kwa kuzingatia kanuni husika.

12. Matayarisho / maandalizi ya somo

Soma kitabu cha mwanafunzi na kiongozi cha mwalimu kwa makini na kukielewa kabla ya kufundisha. Hii itakusaidia kuelewa kwa undani vipengele vyote unavyotakiwa kufundisha. Hakikisha unaandaa somo lako vizuri kama inavyotakiwa. Kumbuka kuchagua mbinu sahihi ya kujifunzia na kufundishia kulingana na maudhui ya somo, mazingira, idadi, uwezo na umri wa wanafunzi, muda na upatikanaji wa vifaa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 10 26/07/2021 12:02

13. Fikiri

Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyoorodheshwa katika kipengele cha *fikiri* katika kila sura kabla ya kusoma. Majibu yao yatakusaidia kuelewa maarifa ya awali aliyonayo mwanafunzi kuhusu sura husika.

14. Mgawanyo wa vipindi

Katika mwaka wa masomo, kuna siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39 za masomo. Makadirio ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Katika darasa hili, kuna vipindi 7 vya Kiswahili kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

15. Mrejesho kwa wanafunzi

Sahihisha kazi zote za wanafunzi na kuwapa mrejesho. Ni vyema kufanya masahihisho darasani ili kila mwanafunzi atambue kosa lake na kujisahihisha.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 11 26/07/2021 12:02

Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kiongozi hiki cha mwalimu. .

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

Waandishi: Mwl. Rose S. Chipindula, Mwl. Melina A. Yohana, Mwl. Samwel M. Magutu, Mwl Tumaini M. Mahendeka na Mwl. Adelgot J. B. Mapunda

Wahariri: Prof. David P. B. Massamba, Dkt. Faraja J. Mwendamseke (Mwenyekiti wa jopo la uhariri wa maudhui) na Bw. Mussa R. Kaoneka (Lugha - BAKITA)

Msanifu: Bw. Kuyonza K. Kuyonza

Wachoraji: Alama Arts and Media Production Limited

Mratibu: Mwl. Rose S. Chipindula

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Vilevile, TET inatoa shukurani za pekee kwa shirika la "Global Partnership for Education (GPE)" kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao "Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)" kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kuchapisha kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 12 26/07/2021 12:02

Sura ya Kwanza

Kuimba wimbo wa kizalendo

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi ataimba wimbo wa Tanzania Tanzania na kujibu maswali kwa ufupi. Pia, ataghani shairi la kizalendo la Tanzania yangu. Lengo kuu ni kumchochea mwanafunzi awe mzalendo kwa nchi yake.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kuimba wimbo wa **Tanzania, Tanzania**
(b) kughani shairi la kizalendo la **Tanzania yangu**
(c) kusoma shairi la **Tanzania yangu** na kujibu maswali

Mahitaji: vitu halisi, chati za maneno, kalamu rashasha, kadi za maneno, kadi za sentensi, picha (za kawaida na za mguso), bangokitita, diski ya nyimbo mbalimbali za kizalendo na ramani ya Tanzania

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali ya *fikiri* yaliyopo ukurasa wa **kwanza** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Lengo la maswali ya fikiri ni kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza pamoja na kupata uelewa wa mwanzo alionao mwanafunzi kuhusu somo utakalofundisha.
(b) Waongoze wanafunzi kuimba wimbo wa Tanzania Tanzania.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi lililopo ukurasa wa **pili** hadi wa **tano** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi katika makundi kujibu maswali yafuatayo:

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 1 26/07/2021 12:02

(i) Kila ubeti wa shairi una mishororo mingapi?
(ii) Katika ubeti wa tatu mwandishi anatoa ujumbe gani?
(iii) Mshairi ametaja mbuga gani za wanyama?
(iv) Unahisi nchi gani ambayo mshairi anajivunia? Kwa nini?

(e) Sikiliza majibu kutoka katika makundi, rekebisha makosa yanapojitokeza.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **5** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kifanyike katika somo hili.
(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma ubeti mmoja au beti mbili za shairi kwa kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao wala uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo. Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 2 26/07/2021 12:02

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika maneno yafuatayo ubaoni: *nudhumu, inda, hayawani, dafina, mithili, saza, kaditama, fichama, adhama* na *fuadi*, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.
(b) Fundisha maneno hayo kwa kutumia mbinu ya vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.
(c) Waongoze wanafunzi kuoanisha msamiati na maana zake kwenye zoezi la pili lililopo ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(d) Waelekeze wanafunzi kusoma msamiati na maana zake.
(e) Angalia usahihi wa msamiati na maana zake.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha msamiati na maana zake ni sahihi.

Majibu:

(i)	*d*	*(iv)*	*h*	*(vii)*	*a*	*(ix)*	*f*
(ii)	*b*	*(v)*	*c*	*(viii)*	*j*	*(x)*	*e*
(iii)	*g*	*(vi)*	*i*				

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.
(b) Tumia mfano uliopo zoezi la 3 ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Ongeza mifano mingine.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **6** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

1. *chombo huenda mrama*
2. *Mzaha mzaha*
3. *usambe ni utajiri*
4. *Penye miti*
5. *muungwana ni kitendo*
6. *Mzoea vya kunyonga*
7. *humrukia*
8. *Aliye* kando
9. *ila kwa ncha ya upanga*
10. *Atafutaye hachoki*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 3 26/07/2021 12:02

Somo la 5: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.

Mfano: Kitendawili -Tega

Natembea walio wafu wanalia na walio hai wametulia - *majani makavu na mabichi.*

Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji anaoupenda ili atoe jibu sahihi.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha na mifano kutega na kutegua kitendawili, kwa mfano onesha picha ya uyoga ili wanafunzi watunge kitendawili: *Nyumba yangu ina nguzo moja - Uyoga*

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **7** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

1. *miguu*
2. *tumbo na kitovu*
3. *moyo*
4. *maji mtoni*
5. *zipu*
6. *nywele*
7. *mbegu*
8. *mzinga wa nyuki*
9. *mzinga na nyuki*
10. *redio*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika maneno yenye maana sawa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno wanayoyafahamu yenye maana sawa na maneno waliyopewa. Tumia mifano iliyopo zoezi la 5 A ukurasa wa **7** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **7** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 4 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) moyo
(ii) tamati/mwisho
(iii) jificha
(iv) saza
(v) asa
(vi) gere/ wivu
(vii) nguli/jasiri
(viii) mstari
(ix) udhi, sumbua, ghasi
(x) laana, maapizo, maangamizo, gharika

B. Kupigia mstari neno lililo tofauti na maneno mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache kwa kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

Mfano:

(i) kaka, dada, mjomba, shangazi, <u>rafiki</u>
(ii) ulezi, uwele, mahindi mtama, <u>papai</u>

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **7 - 8** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) mpasuko
(ii) figo
(iii) saza
(iv) mzaha
(v) rushwa
(vi) kubali
(vii) udongo
(viii) zoleka
(ix) nyamaza
(x) patia
(xi) pindua

C. Kuandika neno sahihi badala ya neno lililokolezwa

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 C ukurasa **8** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza jinsi ya kuandika neno sahihi kwa kuzingatia ufasaha wa sarufi ya Kiswahili.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa **8** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 5 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) wimbo wa
(ii) yeyote
(iii) fedha
(iv) adui
(v) amani
(vi) nchi
(vii) Tunasoma
(viii) Ruaha, shairi
(ix) Lugha, Kiswahili
(x) Mwalimu, vizuri

D. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyo katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jinsi ya kutumia maneno yaliyoko kwenye kisanduku kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

(ii) Toa mifano kwa kujaza maneno sahihi katika sentensi zifuatazo:

Mfano: _____ *amesoma kitabu cha Kiswahili.*
Yeye amesoma kitabu cha Kiswahili.
_____ *tunasoma Hisabati kila siku.*
Sisi tunasoma Hisabati kila siku.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **8** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) rambirambi
(ii) mzalendo
(iii) kaulimbiu
(iv) misitu
(v) bustani
(vi) kibwagizo
(vii) rasilimali
(viii) kusoma
(ix) samani
(x) mtiifu

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 6 26/07/2021 12:02

E. Kuandika NDIYO au HAPANA

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) HAPANA
(ii) NDIYO
(iii) HAPANA
(iv) HAPANA
(v) HAPANA
(vi) NDIYO
(vii) NDIYO
(viii) HAPANA
(ix) NDIYO
(x) NDIYO

F. Kujibu maswali kwa usahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waelekeze wanafunzi jinsi ya kufanya zoezi husika.

(ii) Nakili ubaoni zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Tumia swali la kwanza kama mfano.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) nne (bluu, kijani, nyeusi, njano)
(ii) itategemea majibu kutoka kwa wanafunzi (majibu yawe na uelekeo wa kizalendo)
(iii) kuzitunza na kuzilinda
(iv) kila raia
(v) msaliti

G. Kubadili sentensi zifuatazo kuwa katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Waelekeze wanafunzi kuhusu dhana ya umoja na wingi katika lugha ya Kiswahili.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 7 26/07/2021 12:02

(ii) Toa mifano ya kubadili sentensi zilizo katika umoja kuwa katika wingi.

Mfano: *Mjomba wangu amelima shamba kubwa sana.*
Wajomba zangu wamelima mashamba makubwa sana.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Tamkeni maneno haya kwa ufasaha.
(ii) Ghani mashairi haya kwa mbwembwe.
(iii) Nyimbo hizi zinazitukuza nchi zetu.
(iv) Alama hizi za uandishi ni za muhimu sana katika uandishi.
(v) Sentensi hizi zipo katika wakati uliopo.
(vi) Wanafunzi lazima wafuate ratiba za shule.
(vii) Sare za shule zetu ni mashati ya rangi nyeupe.
(viii) Visima vyangu vimejaa maji tele.
(ix) Paka shume wamemkamata kuku wetu.
(x) Sisi na ndugu zetu ni wazawa wa nchi hizi.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja shughuli zinazofanywa na kiongozi wa darasa lao.

(b) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **9** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa.

(d) Baada ya kusahihisha chagua kazi iliyoandikwa vizuri ili wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 8 26/07/2021 12:02

Sura ya Pili

Shairi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kughani na kubaini mawazo makuu yanayopatikana katika shairi. Pia, atatunga shairi la kimapokeo kwa kuzingatia kanuni za urari wa vina na mizani. Vilevile, ataeleza maana ya taswira zilizomo katika shairi na kuzihusianisha na maisha ya kila siku.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kueleza maana ya shairi
(b) kusoma na kughani shairi
(c) kueleza maana ya vina, mizani, mishororo na ubeti
(d) kueleza mawazo makuu na ujumbe katika shairi
(e) kufafanua maana za taswira katika shairi
(f) kufafanua maana za maneno

Mahitaji: shairi la mfano, matini mbalimbali yenye mashairi, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa wa **10** katika Kitabu cha Mwanafunzi katika kipengele cha *fikiri*. Toa nafasi ya mwanafunzi kughani shairi fupi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi lililopo ukurasa wa **10 - 12** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha vidole wala kutoa sauti.

(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
(i) Shairi linahusu nini ?
(ii) Mwandishi amesisitiza nini katika beti zifuatazo: wa pili, wa tano, wa kumi na wa kumi sita.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 9 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili katika makundi kuhusu lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika shairi hilo.
(e) Waongoze wanafunzi kughani shairi walilolisoma kwa mahadhi tofautitofauti.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **12** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu sahihi za kusoma kwa sauti.
(b) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa shairi kwa kuzingatia kiimbo na hisia.
(c) Wakumbushe wanafunzi kuhusu vina, mizani na mishororo. Wataje vina vya kati na vya mwisho kwa kila ubeti na kuhesabu idadi ya mizani katika kila mstari. Vina ni silabi zinazolingana katikati na mwishoni mwa ubeti wa shairi. Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo.
(d) Washirikishe wanafunzi kutaja vina vya kati na vya mwisho kwa kila ubeti.
(e) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, kwa kuzingatia jinsi. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(f) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza katika usomaji na kuzisahihisha.
(g) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(h) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha matumizi ya msamiati ufuatao: *dawamu*, *sonara, mkumbo, nudhumu, tijara, ving'ora, fukara, dura, hatamu, nira, ghera, ajira, chiriku, ng'amua, mizani, kunguni, azizi, usia, hamasa na charukia.* Tumia mbinu mbalimbali mfano mbinu ya maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 10 26/07/2021 12:02

(b) Andika maneno hayo ubaoni, wanafunzi wayasome na kujadiliana katika makundi madogomadogo, kisha waeleze maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari.
(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mdomo kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na kuangalia kama ziko sahihi. Washirikishe wanafunzi wazisome kwa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **12 - 13** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasisitize kuwa, sentensi watakazozitunga, zisifanane na zile walizotunga katika mifano ya darasani.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazofahamu, wataje mianzo na miisho na kuzikamilisha.
(b) Angalia usahihi wa miisho na mianzo ya methali walizozitaja wanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **13** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) hufa maskini.
(ii) Nyota njema
(iii) Shari hutoka
(iv) hukata huku na huku.
(v) Kuku jike
(vi) ni ujahili.
(vii) hukutania chunguni.
(viii) ni maji.
(ix) Kuzima koleo
(x) Mtaka yote kwa pupa

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari neno lenye maana tofauti na maneno mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.
(ii) Andika maneno yenye maana sawa ubaoni.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 11 26/07/2021 12:02

(iii) Chopeka neno lenye maana tofauti kwenye kifungu husika cha maneno. Ongoza wanafunzi kubaini neno lenye maana tofauti.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **13** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) hadithi (ii) mahindi (iii) mlio (iv) gazeti (v) aya (vi) sahani (vii) chiriku (viii) ulevi (ix) kunguni

B. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika mfano wa swali la kuchagua ubaoni na waongoze wanafunzi kulijibu kwa kujaza herufi ya jibu sahihi.

Mfano: *Idadi ya mizani katika mshororo wa shairi la kimapokeo ni 16:*

(a) 4 (b) 8 (c) 12 (d) 16

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **13 - 15** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i)	*c*	*(vi)*	*c*
(ii)	*a*	*(vii)*	*d*
(iii)	*d*	*(viii)*	*b*
(iv)	*b*	*(ix)*	*b*
(v)	*a*	*(x)*	*d*

C. Kueleza maana ya taswira zilizotumika katika shairi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma shairi.
(ii) Waongoze kubaini taswira zinazojitokeza katika shairi hilo. Washirikishe kutaja taswira zote zilizotumika katika shairi ukurasa wa **15** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 12 26/07/2021 12:02

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza maana za taswira. Wape uhuru kila mmoja kueleza anavyoweza.
(iv) Wagawe wanafunzi kwenye vikundi. Kila kikundi kijadili maana za taswira mbili au zaidi, kisha kila kikundi kitoe maana ya taswira kutokana na mjadala wao.
(v) Ruhusu mjadala mfupi darasani kuhusu taswira hizo. Sahihisha makosa yatakayojitokeza kwa wanafunzi.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C ukurasa wa **15** katika Kitabu cha Mwanafunzi. *(Katika kusahihisha majibu ya maana za taswira usiegemee kwenye jibu moja tu. Pia, angalia wazo la mwanafunzi kama liko sahihi).*

Majibu:

(i) kusoma kwa bidii/ kuhudhuria vipindi
(ii) mitihani/kalamu na daftari
(iii) darasa/sehemu ya kufanyia mazoezi ya kielimu
(iv) magenge au vikundi visivyo na malengo mazuri ya maisha/ urafiki wa kupotezeana muda
(v) silaha imara ya kumpitisha mtu kwenye hatari
(vi) kifaa kinachohakiki ubora wa taaluma
(vii) mtu mnyonyaji/asiye na faida
(viii) kibaka, asiye na mwelekeo
(ix) mtu asiye mwaminifu, mdokozi
(x) mamlaka/sheria

D. Kutunga sentensi kumi (10) kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo katika zoezi la 4 D ukurasa wa **15** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyopo kwenye jedwali.
(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi tano kama mifano.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 13 26/07/2021 12:02

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **15** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

E. Kuandika wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Ongoza wanafunzi kutaja majina ya vitu mbalimbali na uyaandike ubaoni.

(ii) Waongoze wanafunzi kuandika umoja na wingi wa maneno waliyoyataja.

(iii) Waongoze wanafunzi kujadili jinsi ya kuandika umoja na wingi wa maneno yafuatayo: ng'ombe, punda, shule, chumba.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **16** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) mbuzi
(ii) mashairi
(iii) elimu
(iv) misumeno
(v) miezi
(vi) beti
(vii) nchi
(viii) masonara
(ix) ving'ora
(x) nira

F. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Ongoza wanafunzi kufafanua dhana ya ukanushi kwa kutumia mifano.

(ii) Waongoze wanafunzi watunge sentensi. Andika sentensi hizo ubaoni, kisha washirikishe wanafunzi wazikanushe. Andika ubaoni majibu ya wanafunzi, kisha washirikishe kurekebisha makosa yanayojitokeza.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **16** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 14 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) Shairi haliigizwi.
(ii) Nikiwa mkubwa sitakuwa mcheza masumbwi.
(iii) Baba hana kiwanda cha sabuni.
(iv) Shairi si lazima liwe na beti kumi.
(v) Kiswahili si lugha ya kigeni Tanzania.
(vi) Sijapata maswali yote.
(vii) Mwanafunzi hasomi kamusi ya Kiswahili.
(viii) Nyumbani kwetu si mbali.
(ix) Eva hapalilii bustani ya babu yake.
(x) Mwandiko mzuri si wa Chausiku tu.

G. Kupanga herufi zilizochanganywa ili zilete neno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja maneno na uyaandike ubaoni. Changanya herufi za maneno hayo na uziandike ubaoni.
(ii) Shirikisha wanafunzi kupangilia herufi za maneno hayo ili kuleta neno sahihi na uliandike ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **16 - 17** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) nasaha
(ii) tamati
(iii) kalamu
(iv) charuka
(v) nguli
(vi) darasa
(vii) mkumbo
(viii) viwanda
(ix) teknolojia
(x) dadisi

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 15 26/07/2021 12:02

H. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika sentensi zenye nafasi wazi, kisha ushirikishe wanafunzi kuzijaza. Andika maneno ya kuchagua angalau matatu kwa kila swali. *(Unaweza kutumia mbinu ya maswali na majibu au mbinu nyingine)*

(ii) Waongoze wanafunzi kujaza nafasi wazi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kila swali.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **17** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *wanapenda*
(ii) *alimkuta*
(iii) *anaitwa*
(iv) *nitakwenda*
(v) *anahimiza*
(vi) *atajenga*
(vii) *asingalikuwa*
(viii) *ameondoka*
(ix) *tunakwenda*
(x) *nilisoma*

I. Kuoanisha maelezo kutoka sehemu B na kuyatumia kukamilisha sentensi katika maelezo ya sehemu A kwa kuandika herufi ya jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sehemu A na sehemu B.

(iii) Waongoze wanafunzi kuoanisha sehemu hizo kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 4 I lililopo ukurasa wa **18** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 I lililopo ukurasa wa **18** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 16 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*h*	*(vii)*	*d*
(ii)	*f*	*(viii)*	*a*
(iii)	*k*	*(ix)*	*b*
(iv)	*c*	*(x)*	*e*
(v)	*i*	*(xi)*	*j*
(vi)	*l*	*(xii)*	*g*

Somo la 6: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Toa mifano ya nahau na uwaongoze wanafunzi kueleza / kupata maana za nahau ulizoandika.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali wanazozifahamu na kueleza maana zake.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **18 - 19** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) chukua kitu au mtu kwa nguvu

(ii) kuwa na mamlaka

(iii) pata kibali au ruhusa

(iv) weka mashakani

(v) mfanye mtu asikate tamaa

(vi) jivike vazi zuri na jipya

(vii) fanya uamuzi kwa muda mwafaka bila kukawia

(viii) kuwa kigeugeu

(ix) takiana heri

(x) tembea bega kwa bega au ubavu kwa ubavu

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 17 26/07/2021 12:02

Somo la 7: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

(b) Soma kwa makini kifungu cha habari kwa kuzingatia matamshi fasaha ya Kiswahili huku wanafunzi wakisikiliza.

Siku hizi vijana wengi wanalalamika kuhusu ukosefu wa ajira. Wapo vijana wachache sana wanaotambua ajira zitokanazo na kazi za sanaa. Taaluma ya mashairi ni moja kati ya taaluma zinazotoa ajira kwa vijana wa jinsi zote. Vyombo vya habari vinaajiri vijana wenye umahiri wa kutunga na kughani mashairi. Vijana werevu wameanza kuchangamkia taaluma ya mashairi wangali wadogo.

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa na usafi wa kazi.

Somo la 8: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi lililopo ukurasa wa **19 - 20** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha kwa vidole wala kutoa sauti.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 18 26/07/2021 12:02

(b) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:

(i) Shairi ulilosoma lina jumla ya beti ngapi?

(ii) Kila ubeti wa shairi ulilosoma una mishororo mingapi?

(iii) Shairi linahusu nini?

(iv) Kwa nini mtunzi amesisitiza maadili?

(c) Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu lugha ya picha (taswira) iliyotumika katika shairi hilo.

(d) Waongoze wanafunzi kughani shairi walilolisoma.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **20** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 9: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na utaratibu sahihi wa kusoma kwa sauti.

(b) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa shairi kwa kuzingatia kiimbo na hisia.

(c) Wakumbushe wanafunzi kuhusu vina, mizani na mishororo kwa kuwaongoza wataje vina vya kati na vya mwisho kwa kila ubeti na kuhesabu idadi ya mizani katika kila mstari. Vina ni silabi zinazolingana katikati na mwishoni mwa ubeti wa shairi. Mizani ni idadi ya silabi katika mstari wa ubeti.

(d) Washirikishe wanafunzi kutaja vina vya kati na vya mwisho kwa kila ubeti.

(e) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu kwa kuzingatia jinsia. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(f) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza katika usomaji na kuzisahihisha.

(g) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(h) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 19 26/07/2021 12:02

Somo la 10: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha maana na matumizi ya msamiati ufuatao: *mikasa, takabari, hadaa, utu, tunu, ufa, hila, jambia, koroma, karima, chutama, mkunga, nanga* na *dahari*.

(b) Tumia mbinu mbalimbali mfano mbinu ya maelezo, mjadala, maswali na majibu, igizo au mbinu nyinginezo.

(c) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mdomo kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni na angalia kama ziko sahihi. Washirikishe wazisome kwa sauti.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **20** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile walizotunga kama mfano darasani.

Somo la 11: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga shairi la mapokeo.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili mambo waliyoyataja.

(c) Rekebisha makosa yaliyojitokeza kisha waruhusu wanafunzi kutunga shairi.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 lililopo ukurasa wa **20** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 20 26/07/2021 12:02

Sura ya Tatu

Igizo la elimu ya biashara

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza elimu ya biashara. Atasoma igizo na kuliigiza. Pia, ataeleza wazo kuu na fundisho katika igizo hilo. Vilevile, atajifunza kauli mbalimbali zinazotumika katika lugha, kisha atafanya mazoezi mengine ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma igizo linaloitwa **Elimu ya biashara**
(b) kueleza maudhui yaliyo katika igizo na kuchambua wazo kuu
(c) kuigiza igizo
(d) kubadili sentensi katika kauli mbalimbali za utendaji katika kitenzi

Mahitaji: vitu halisi, mazingira halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati, bangokitita, diski za maigizo (sidii za maigizo), projekta, televisheni, deki, kinyonyi na kompyuta

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo kwenye kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **21** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo katika ukurasa wa **22** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya igizo linaloitwa **Elimu ya Biashara** lililopo ukurasa wa **21 - 24** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia igizo walilolisoma kwa maneno machache.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 21 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Waongoze kufanya swali la 1 - 4 kwa mazungumzo na swali la 5 -10 waandike kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na utaratibu sahihi wa kusoma kwa sauti.

(b) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia. Zingatia usomaji wa majibizano kwa kubadili sauti kwa kila mhusika.

(c) Chagua wanafunzi wasome kwa kuzingatia wahusika wote waliopo kwenye igizo.

(d) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(e) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo papo hapo.

(f) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Kazi ya kufanya (Igizo)

Hatua za ufundishaji

(a) Teua wahusika kwa kuzingatia wahusika waliopo kwenye igizo lililopo ukurasa wa **21 - 24** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Toa maelekezo kwa wahusika.

(c) Wape muda wahusika kujiandaa na kuigiza igizo darasani.

(d) Fanya hitimisho la igizo na wapongeze waigizaji.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 22 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika misamiati ifuatayo ubaoni: *jukwaa, waigizaji, elimu, biashara, sheheni, lukuki, soga, faida, ujuzi, mtaji* na *wateja* na, kisha wanafunzi wasome neno mojamoja na kutamka sauti zinazounda neno hilo.

(b) Fundisha maneno hayo kwa kutumia mbinu ya maelezo, picha na maigizo.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo, kisha waulize maana ya neno ulilolitungia sentensi.
Mfano: Waigizaji wote walijitambulisha jukwaani. Neno jukwaa lina maana gani?

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **24** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa katika mfano.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kubadili sentensi kuwa katika kauli za kutendewa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa kuwa mabadiliko yatafanyika katika kitenzi. Kumbuka kauli ya kutendewa ina kauli mbili ndani yake. Nazo ni kauli ya kutendea na kauli ya kutendwa. Kauli ya kutendea huoneshwa kwa kutumia herufi -e-, -i- na silabi -le- na -li-. Kauli ya kutendwa huoneshwa kwa kutumia herufi -w-. Herufi zinazoonesha utendea, hutangulia. Hufuatiwa na herufi inayoonesha utendwa. Herufi zinazoonesha utendea na utendwa huwekwa baada ya mzizi wa kitenzi kabla ya irabu ya mwisho katika kitenzi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 A lililopo kwenye ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 23 26/07/2021 12:02

B. Kubadili vitendo kuwa katika kauli ya kutendeka

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa kuwa mabadiliko yatafanyika katika kitenzi. Kumbuka kauli ya kutendeka huwa na herufi k kabla ya irabu ya mwisho katika kitenzi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 B lililopo kwenye ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

C. Kubadili vitenzi kuwa katika kauli za kutendwa, kutendea, kutendewa, kutendeana, kutendesha, kutendana na kutendeka

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa kuwa mabadiliko yatafanyika katika herufi za mwisho baada ya mzizi wa vitenzi. Herufi zitakazotumika ni -w-, -i-/-e-, -iw-/-ew-, -ian-/-ean-, -ish-/esh-, -an- , -ek-/-ik- na kumalizia na irabu tamati katika kitenzi husika.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 C lililopo kwenye ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **25** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

Na	kutenda	kutendwa	kutendea	kutendewa	kutendeana	kutendesha	kutendana	kutendeka
(i)	andika	Andikwa	Andikia	Andikiwa	Andikiana	Andikisha	Andikana	andikika
(ii)	kusanya	kusanywa	kusanyia	kusanyiwa	kusanyiana	kusanyisha	kusanyana	kusanyika
(iii)	peleka	pelekwa	pelekea	pelekewa	pelekeana	pelekesha	pelekana	pelekeka
(iv)	kanda	kandwa	kandia	kandiwa	kandiana	kandisha	kandana	kandika
(v)	funga	fungwa	fungia	fungiwa	fungiana	fungisha	fungana	fungika
(vi)	chunga	chungwa	chungia	chungiwa	chungiana	chungisha	chungana	chungika
(vii)	sema	semwa	semea	semewa	semeana	semesha	semana	semeka

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 24 26/07/2021 12:02

(viii)	chora	chorwa	chorea	chorewa	choreana	choresha	chorana	choreka
(ix)	tazama	tazamwa	tazamia	tazamiwa	tazamiana	tazamisha	tazamana	tazamika
(x)	piga	pigwa	pigia	pigiwa	pigiana	pigisha	pigana	pigika

D. Kuunganisha sentensi kwa kutumia irabu “u” na “e” bila kutumia kiunganishi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zote.

(ii) Toa maelezo kuhusu jinsi ya kuunganisha sentensi hizo mbili kwa kutumia irabu u na e. Kitenzi cha pili utaanza na irabu u na mwisho wa kitenzi utaiondoa irabu a na kuweka irabu e.

(iii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 D lililopo kwenye ukurasa wa **26** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **26** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) Fungua mlango, ungie ndani.
(ii) Vaa miwani, usome sentensi hizi.
(iii) Igiza igizo, ushangiliwe kwa mbwembwe.
(iv) Chota maji, umimine kwenye pipa.
(v) Nenda sokoni, ununue nyanya.
(vi) Pukuchua mahindi, uweke kwenye gunia.
(vii) Fuga nyuki, urine asali.
(viii) Andika barua, utume kwa njia ya posta.
(ix) Soma kwa bidii, ufanikiwe katika maisha yako.
(x) Ongea Kiswahili fasaha, ukuze lugha ya Taifa.

E. Kubainisha kauli za utendaji katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 E kwenye ukurasa wa **26** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **26** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 25 26/07/2021 12:02

F. Kujaza nafasi zilizo wazi katika jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa kuwa mabadiliko yatafanyika katika viambishi tamati vya kitenzi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 F lililopo kwenye ukurasa wa **27** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **27** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

Na	kutenda	kutendwa	kutendewa	kutendeana	kutendea	kutendeka
(i)	tupa	tupwa	tupiwa	tupiana		tupika
(ii)	imba	imbwa	imbiwa		imbia	imbika
(iii)		katwa	katiwa	katiana	katia	katika
(iv)		rukwa	rukiwa	rukiana	rukia	rukika
(v)		tekwa	tekewa	tekeana	tekea	tekeka

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya somo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji na yaandike ubaoni.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo kwenye ukurasa wa **27** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na herufi kubwa. Zingatia usahihi wa matumizi ya nafsi, nyakati na mnyumbuliko wa vitenzi.

(e) Baada ya kusahihisha, chagua habari iliyoandikwa vizuri na wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 26 26/07/2021 12:02

Sura ya Nne

Hadithi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusimulia hadithi yenye methali, mianzo na miisho ya hadithi na kuelezea mafunzo yaliyopo kwenye hadithi hizo. Vilevile, atajifunza methali nyingine zenye maana zinazofanana na methali zilizotajwa katika hadithi. Pamoja na hayo, atajifunza methali nyingine zenye maana iliyo kinyume.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi ya **Umoja ni nguvu**
(b) kueleza maana ya methali
(c) kukamilisha methali
(d) kueleza na kuhusisha methali na umuhimu wa kuheshimu kazi

Mahitaji: vitu halisi, chati za methali na picha (za kawaida na za mguso)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa **28** kwenye kipengele cha *Fikiri* katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Umoja ni nguvu** iliyopo ukurasa wa **28 - 31** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
  (i) Taja majina ya watu waliotajwa katika hadithi.
  (ii) Je, ni methali zipi ulizozisoma kwenye hadithi?

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie hadithi waliyoisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **32** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 27 26/07/2021 12:02

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza unachotarajia kifanywe katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanaposoma na kuzirekebisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *uashi/mwashi, useremala/seremala*, *kibarua, ujira, hamaki, makamo, sabahi, dodosa, duwaa, ubinafsi/mbinafsi, tanda, ng'aka* na *ghadhabu* kwa kutumia maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome. Waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **32** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa kama mfano na zilizotumika kitabuni.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 28 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kueleza maana za methali

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.
(ii) Hakikisha methali zilizotajwa na wanafunzi ni sahihi.
(iii) Andika methali hizo ubaoni.
(iv) Kagua usahihi wa methali zilizotajwa na wanafunzi.
(v) Waongoze wanafunzi kueleza maana za methali walizozitaja
(vi) Tumia mfano uliopo zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **32** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Ongeza mifano mingine.
(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **32 - 33** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Si vizuri kufanya mambo kwa pupa.
(ii) Jambo linalofanywa kwa pupa halifanikiwi.
(iii) Mwenzako akifikwa na tatizo au shida unapaswa kujitayarisha au kuchukua tahadhari ili usije ukakumbwa na shida kama hiyo.
(iv) Watu walio mahali palipo na vitu fulani vya thamani kwa wingi, mara nyingi huwa hawavitumii au hawavithamini.
(v) Jambo la heri likikufikia, unapaswa kulifurahia.
(vi) Ni muhimu kufanya kazi hata kama ni mbaya au duni kuliko kutofanya kazi kabisa. Kazi yoyote halali humletea mtu manufaa, lakini kujikalia bwete hakumfaidishi mtu.
(vii) Jambo fulani linapotaka kutokea, ishara zake huonekana kwanza kuashiria kwamba jambo hilo litatokea.
(viii) Tabia ya kujivuna au kuringa si nzuri.
(ix) Tusiruhusu kutawaliwa na hasira au kufanya mambo tukiwa tumekasirika kwani matokeo yake yanaweza kutusababishia hasara.
(x) Usifanye jambo ukiwa umekasirika kwa kuwa matokeo yake yanaweza kuwafaidisha watu wengine na kukusababishia hasara.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 29 26/07/2021 12:02

(xi) Jambo ambalo limeandikiwa kuharibika, litaharibika tu hata kama utafanya juhudi nyingi za kulinusuru.

(xii) Mungu hana upendeleo kama binadamu. Binadamu anaweza kumwombea maovu binadamu mwenzake, lakini Mungu anao uwezo wa kumnusuru na uovu huo.

(xiii) Tusifanye mambo ovyoovyo pasipo kutafakari kwa makini kwani tukifanya hivyo, tunaweza kuyajutia baadaye.

(xiv) Ni muhimu kushirikiana na binadamu wenzako maishani katika mambo mbalimbali kwani kufanya hivyo kuna faida nyingi.

B. Kuchagua methali katika kisanduku, kisha kuiandika mbele ya maelezo yanayoendana nayo

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja kwa usahihi methali wanazozifahamu.

(ii) Ziandike methali hizo ubaoni.

(iii) Sahihisha makosa mara tu yanapojitokeza.

(iv) Tumia mfano uliopo zoezi la 3 B ukurasa **33** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa **33 - 34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Chanda chema huvikwa pete.

(ii) Fedha fedheha.

(iii) Fimbo ya mnyonge hulipwa na Mungu.

(iv) Penye nia pana njia.

(v) Hasara humfika mwenye mabezo.

(vi) Heri jirani karibu kuliko ndugu mbali.

(vii) Kazi isiyo na manufaa kutenda si inda.

(viii) Cha mlevi huliwa na mgema. / Fedha fedheha. / Hasara humfika mwenye mabezo.

(ix) Msahau kwao ni mtumwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 30 26/07/2021 12:02

C. Kuoanisha maneno kutoka sehemu A na vinyume vyake kutoka sehemu B

Hatua za ufundishaji

(i) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili yenye mchanganyiko wa wavulana na wasichana.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma katika makundi sehemu A na sehemu B

(iii) Kundi moja wasome maneno yaliyopo sehemu A na kundi lingine wasome vinyume vyake kutoka sehemu B.

(iv) Waongoze wanafunzi kuoanisha maneno na vinyume vyake.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **34** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*h*	*(vi)*	*b*
(ii)	*k*	*(vii)*	*j*
(iii)	*f*	*(viii)*	*e*
(iv)	*l*	*(ix)*	*g*
(v)	*c*	*(x)*	*i*

D. Kuandika methali kumi (10) sahihi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo zoezi la 3 D ukurasa wa **35** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma kwa pamoja safu ya kwanza, ya pili na ya tatu katika jedwali.

(iii) Ongoza mwanafunzi mmojammoja kusoma safu ya kwanza, ya pili na ya tatu katika jedwali.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **35** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 31 26/07/2021 12:02

E. Kuchagua jibu lililo sahihi na kuandika herufi yake katika kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuchagua jibu sahihi kwa kutumia swali la kwanza kama mfano lililopo zoezi la 3 E, ukurasa wa **35**, katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **35 - 37** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*a*	*(iv)*	*a*	*(vii)*	*d*	*(x)*	*b*
(ii)	*b*	*(v)*	*d*	*(viii)*	*a*	*(xi)*	*c*
(iii)	*a*	*(vi)*	*c*	*(ix)*	*c*	*(xii)*	*a*

F. Kumalizia methali

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu zoezi litakalofanywa.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu. Hakikisha kuwa methali zilizotajwa na wanafunzi ni sahihi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **37** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*huvunjika guu*	*(vi)*	*kibindoni*
(ii)	*usambe ni utajiri*	*(vii)*	*mguu huota tende*
(iii)	*lisingoje kesho*	*(viii)*	*kibaya chajitembeza*
(iv)	*mchawi*	*(ix)*	*utamkuta mwana si wako*
(v)	*kuliko maji*	*(x)*	*halina ubani*

G. Kuandika methali zenye maana sawa

Hatua za Ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma methali zilizopo katika zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **37** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **37** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Tumia majibu yafuatayo kama mfano.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 32 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) Hakuna marefu, yasiyokuwa na ncha.
(ii) Mwenda mbio, hujikwaa dole.
(iii) Chelewa chelewa, utamkuta mwana si wako.
(iv) Majuto ni mjukuu.
(v) Majuto hayatangulii.
(vi) Baada ya dhoruba, huja utulivu.
(vii) Heri ya mrama, kuliko ya kuzama.
(viii) Ukitaka cha uvunguni, sharti uiname.
(ix) Ng'ombe wa maskini, hazai mapacha.
(x) Baada ya kifo ni tabibu.

H. Kuandika neno moja linalojumuisha maneno yaliyo katika mabano

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo unalotaka kufundisha.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyo katika mabano kwenye zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **37 - 38** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **37 - 38** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *vyombo*
(ii) nguo
(iii) vyakula
(iv) matunda
(v) nafaka
(vi) samani
(vii) silaha
(viii) vinywaji
(ix) mzalendo
(x) samaki

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(b) Ongoza majadiliano kuhusu uhusiano uliopo kati ya methali na vitu vilivyopo katika mazingira ya mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **38** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi, mtiririko wa mawazo na matumizi ya methali.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 33 26/07/2021 12:02

Sura ya Tano

Taswira za nahau

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kutumia nahau katika habari fupi. Pia, atajifunza kutafsiri taswira zilizomo katika nahau hizo. Vilevile, atajifunza msamiati, miundo na nahau zilizomo katika habari. Aidha, atafanya mazoezi mbalimbali ya lugha, kazi ya kufanya pamoja na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi kuhusu **Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika**
(b) kutaja nahau wanazozifahamu
(c) kueleza taswira za kimawazo zilizomo katika nahau
(d) kutunga habari fupi kwa kutumia nahau

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), diski na chati ya nahau, kalamu rashasha na bangokitita

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **39** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari fupi ya **Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika** iliyopo ukurasa wa **39 - 41** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalifanyika wapi?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 34 26/07/2021 12:02

(ii) Kwa nini Nyamate alimwachisha Upendo shule?

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **40** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Maswali yafuatayo yatakuongoza.

(i) Wanafunzi wanafanya nini?

(ii) Wengine ni akina nani?

(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza ukurasa wa **42** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 35 26/07/2021 12:02

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *adhimisha, nidhamu, tumbuiza, haki, tuzo, kidete, yaya* na *hamaki* kwa kutumia vitu halisi, maelezo, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili ukurasa wa **42** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazozitunga hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau zilizotumika katika habari ya **Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika** ukurasa wa **42 - 43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Andika ubaoni nahau walizozitaja wanafunzi.

(c) Angalia usahihi wa nahau zilizotajwa na wanafunzi.

(d) Waongoze wanafunzi kueleza taswira za kimawazo zilizomo katika nahau hizo kwa kutoa mifano.
Mfano: *pigwa chini - fukuzwa kazi*

(e) Waongoze wanafunzi kutaja nahau zingine zinazoleta taswira hizohizo.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 ukurasa wa **42 - 43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 36 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*m*	*(v)*	*p*	*(ix)*	*a*	*(xiii)*	*h*
(ii)	*o*	*(vi)*	*k*	*(x)*	*g*	*(xiv)*	*l*
(iii)	*n*	*(vii)*	*c*	*(xi)*	*b*	*(xv)*	*f*
(iv)	*e*	*(viii)*	*j*	*(xii)*	*i*		

Somo la 5: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 4 ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.

(d) Waelekeze wanafunzi kanuni za miundo ya ... *ndani ya ...,* *... juu ya..., ... chini ya ..., katikati ya ...* na ... *mbele ya ...*

(e) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 4 ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na ziandike sentensi hizo ubaoni.

(g) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **43** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 37 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) wageni *(iv) kiwanda* *(vii) masomo* *(x) kikundi*
(ii) vicheko *(v) mashairi* *(viii) shule*
(iii) risala *(vi) chandarua* *(ix) mazingira*

B. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila kinyume chake.

Mfano: *Mwanafunzi……..*

Swali……

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iii) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.

(iv) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) mwenyeji *(iv) ruhusu* *(vii) mzee* *(x) sasa*
(ii) rahisi *(v) wahi* *(viii) mwerevu*
(iii) dhuluma *(vi) haramu* *(ix) masika*

C. Kuandika sentensi katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Waelekeze wanafunzi kuhusu somo hili. Mwanafunzi azingatie silabi *-ta-* inayoonesha wakati ujao katika kitenzi.

(ii) Toa mfano uliopo katika zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 38 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) Tutakuwa tayari kupigania haki zetu.
(ii) Afisa Maendeleo wa Wilaya atawapa wanafunzi zawadi.
(iii) Wanafunzi wote wataangua kicheko.
(iv) Chausiku atauliza swali darasani.
(v) Mwalimu atawatangazia wanafunzi siku ya Mtoto wa Afrika.
(vi) Vikundi vya ngoma vitaburudisha wanafunzi.
(vii) Nyamate atamwamsha Upendo ili aende shuleni.
(viii) Mgeni rasmi atatangaza kutoa zawadi.
(ix) Mkulima atakwenda shambani.
(x) Watoto wataimba nyimbo nzuri sana.

D. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 5 D ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi kukanusha sentensi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D ukurasa wa **44** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Mwalimu Sikujua hakwenda mjini kutembea.
(ii) Lushinge hakumfukuza Upendo darasani.
(iii) Walimu hawakuwagawia wanafunzi vitabu vya kujisomea.
(iv) Upendo hakukubali kwenda kuchunga ng'ombe.
(v) Maktaba si sehemu ya kutibia wagonjwa.
(vi) Luhumbika hajaimba shairi.
(vii) Mgeni rasmi hatafika kesho asubuhi.
(viii) Wanafunzi hawatashiriki katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Uhuru.
(ix) Mimi sisomi kitabu cha hadithi.
(x) Mwalimu wetu si mgonjwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 39 26/07/2021 12:02

E. Kutunga sentensi sahihi kumi (10) kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita jedwali la zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **45** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyomo kwenye jedwali.
(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kutoka kwenye jedwali kwa mazungumzo.
(iv) Andika ubaoni sentensi zilizotungwa.
(v) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.
(vi) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo kwa sauti.
(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **45** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Wazazi walikuwa wanasoma vitabu.
(ii) Wazazi walikuwa wanawatumbuiza wanafunzi.
(iii) Wazazi walikuwa wanacheza mpira.
(iv) Wazazi walikuwa wanakula chakula.
(v) Mwalimu wetu alikuwa anahutubia.
(vi) Mwalimu wetu alikuwa anafundisha kusoma.
(vii) Mwalimu wetu alikuwa anaimba shairi.
(viii) Mwalimu wetu alikuwa anasoma gazeti.
(ix) Mwalimu wetu alikuwa analima shambani.
(x) Mwalimu wetu alikuwa anatoa huduma ya kwanza.
(xi) Mwalimu wetu alikuwa anamwadhibu mwanafunzi.
(xii) Wacheza ngoma walikuwa wanasoma vitabu.
(xiii) Wacheza ngoma walikuwa wanawatumbuiza wanafunzi.
(xiv) Wacheza ngoma walikuwa wanacheza mpira.
(xv) Wacheza ngoma walikuwa wanakula chakula.
(xvi) Mwanafunzi alikuwa anahutubia.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 40 26/07/2021 12:02

(xvii) Mwanafunzi alikuwa anafundisha kusoma.
(xviii) Mwanafunzi alikuwa anaimba shairi.
(xix) Mwanafunzi alikuwa anasoma gazeti.
(xx) Mwanafunzi alikuwa analima shambani.
(xxi) Mwanafunzi alikuwa anatoa huduma ya kwanza.

F. Kubadili sentensi kuwa katika kauli ya kutendwa

Hatua za ufundishaji

(i) Andika sentensi zifuatazo ubaoni.

Mama amepika chakula.
Wanakijiji walisoma risala.
Rehema anasoma kitabu cha Kiswahili.

(ii) Wafafanulie wanafunzi kuwa sentensi hizo zipo katika kauli ya kutenda.
(iii) Waongoze wanafunzi watunge sentensi zilizo katika kauli ya kutenda.
(iv) Andika sentensi hizo ubaoni.
(v) Waongoze wanafunzi wataje *mtenda*, *kitenzi* na *mtendwa* katika sentensi hizo.
(vi) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi hizo ziwe katika kauli ya kutendwa. Zingatia: sentensi ianze na mtendwa ikifuatiwa na kitenzi kilichopachikwa herufi (-w-) pamoja na kiunganishi "*na"* na kuishia na mtenda. Pia, zingatia wakati wa kitenzi.

Mfano:

(a) Mama amepika chakula.
Chakula kimepikwa na mama.

(b) Wanakijiji walisoma risala.
Risala ilisomwa na wanakijiji.

(c) Rehema anasoma kitabu cha Kiswahili.
Kitabu cha Kiswahili kinasomwa na Rehema.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **45** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 41 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) *Wanafunzi wanafundishwa na mwalimu.*
(ii) *Kitabu kinasomwa na baba yangu.*
(iii) *Mlango ulifunguliwa na dada.*
(iv) *Kitabu changu kimechanwa na Manyama.*
(v) *Basi la shule litaendeshwa na dereva.*
(vi) *Wageni walisalimiwa na Mzee Salimu.*
(vii) *Bustani ilikuwa inapaliliwa na Mafuru.*
(viii) *Mayai mengi yanauzwa na babu yetu.*
(ix) *Vitabu vichache vimesomwa na Zawadi.*
(x) *Mlango wa nyumba yetu umetengenezwa na fundi.*

Somo la 7: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kwa kuwapa kazi ya kutafuta nahau zinazotumika katika mazingira ya jamii yao. Pia, wanaweza kusoma kutoka kwenye vitabu au kuuliza walimu, wanafunzi wenzao, wazazi au walezi wao.
(b) Waongoze wanafunzi watoe nahau hizo kwa kuzungumza.
(c) Andika nahau hizo ubaoni.
(d) Waongoze kusoma nahau hizo.
(e) Waongoze kueleza taswira za kimawazo zilizomo katika nahau katika zoezi la 6 ukurasa wa **45** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(f) Andika ubaoni taswira zilizomo katika nahau hizo.
(g) Waongoze wanafunzi kufafanua taswira zilizomo katika nahau hizo.
(h) Waongoze wanafunzi waandike nahau na taswira zilizomo kwenye nahau hizo kwenye madaftari yao.
(i) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi. Fanya masahihisho pale panapohitajika.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 42 26/07/2021 12:02

Somo la 8: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

(b) Soma kwa makini kifungu cha habari huku wanafunzi wakisikiliza.

Paka na Panya walikuwa marafiki. Siku moja, Panya alimwambia Paka amwachie watoto wake ili awalinde yeye akatafute chakula. Paka alikubali. Panya alimwachia Paka watoto wake na kuondoka. Baada ya Panya kuondoka, Paka alianza kumezea mate watoto wa Panya. Alikata shauri na kushika watoto wa Panya na kuanza kuwala mmoja baada ya mwingine. Panya aliporejea nyumbani, hakuona watoto wake. Alimuuliza Paka, "Watoto wangu wako wapi?" Paka alimjibu kuwa ameshikwa na njaa na amewala wote. Panya aliangua kilio na kujilaumu kwa nini amemwachia Paka watoto wake. Tangu siku hiyo urafiki wa paka na panya ulikwisha.

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.

(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa na usafi wa kazi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 43 26/07/2021 12:02

Somo la 9: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kuandika habari katika mtiririko mzuri.

(b) Nakili ubaoni mwanzo wa habari iliyopo ukurasa wa **45** katika kitabu cha mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma mwanzo wa habari iliyoandikwa ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia habari kwa kutumia nahau zilizotolewa katika zoezi la 7 ukurasa wa **45** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia, alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, matumizi sahihi ya herufi kubwa na matumizi sahihi ya nahau walizopewa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 44 26/07/2021 12:02

Sura ya Sita

Ziara

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma habari inayohusu Ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo. Pia, ataweza kusimulia mambo aliyoyaona katika ziara hiyo fupi. Vilevile, atajifunza msamiati, vitendawili, methali, miundo, mazoezi mbalimbali ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari kuhusu **Ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo** na kujibu maswali ya ufahamu
(b) kufanya ziara katika mazingira ya shule ya jirani
(c) kusimulia mambo atakayojifunza katika ziara
(d) kuandika habari fupi kutokana na mambo aliyojifunza katika ziara

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya msamiati, kalamu na daftari

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **46** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Ziara ya kitaaluma katika Shule ya Msingi Matomondo** iliyopo ukurasa wa **46 - 48** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Mwalimu Matokeo aliwaandalia wanafunzi nini?
    (ii) Mwalimu Mangala aliwaonesha wanafunzi nini?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 45 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **47** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi wasimulie kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **48 - 49** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *ahidi*, *ushirikiano, kumbusha, nadhifu, zuru, ukarimu, nidhamu, maendeleo, maktaba, maarifa na bwalo* kwa kutumia vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.
(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.
(c) Waongoze wanafunzi kuoanisha msamiati na maana zake kwenye zoezi la pili lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 46 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kutamka msamiati na maana zake kwa kuzungumza. Hakikisha unaangalia usahihi wa msamiati na maana zake.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **49** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha msamiati na maana zake ni sahihi.

Majibu:

(i)	*c*	*(vii)*	*i*
(ii)	*d*	*(viii)*	*h*
(iii)	*g*	*(ix)*	*j*
(iv)	*b*	*(x)*	*f*
(v)	*k*	*(xi)*	*a*
(vi)	*e*		

Somo la 4: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.

Mfano: Kitendawili -Tega

Twamsikia lakini hatumwoni - *Sauti*

Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji ili atoe jibu sahihi.

(b) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha na mifano kutega na kutegua vitendawili, kwa mfano:

Anataga huku akitembea - *maboga*

Ubwabwa wa mwana mtamu - *usingizi*

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 47 26/07/2021 12:02

Majibu:

1. *moto*
2. *ngoma*
3. *ndege*
4. *redio*
5. *kioo*
6. *kobe*
7. *popo*
8. *mchwa*
9. *kitanda*
10. *muwa*

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu methali.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(c) Ziandike ubaoni methali hizo.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia methali kwa kutumia swali la mfano lililopo zoezi la 4 ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi kama mfano.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **50** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

1. *Vita ya panzi*
2. *kwenye kuku wengi*
3. *agana na nyonga*
4. *Pilipili usiyoila*
5. *huumiza mkonowe*
6. *Mtoto mkaidi hafaidi*
7. *Liwezekanalo leo*

Somo la 6: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 5 ukurasa wa **50 - 51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.

(d) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 5 ukurasa wa **50 - 51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni. Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 48 26/07/2021 12:02

(f) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **50 - 51** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine katika orodha

Hatua za ufundishaji

(i) Andika orodha ya maneno ambayo ni ya mfano ubaoni kutoka kwenye zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma orodha ya maneno hayo kutoka ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kutaja neno ambalo ni tofauti na mengine kwa kila orodha.
(iv) Pigia mstari neno hilo wakishalitaja.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi kisha waandike katika madaftari yao.

Majibu:

(i) *ghasia, fujo, vurugu, vurumai, muziki*
(ii) *kuona, kusikia, kunusa, kuonja, kupima*
(iii) *gari, treni, basi, pikipiki, ndege*
(iv) *chaki, kitabu, mwanafunzi, kalamu, daftari*
(v) *ndizi, papai, fenesi, nazi, embe*
(vi) *papa, kambare, sangara, perege*
(vii) *simba, tembo, pundamilia, faru, ng'ombe*
(viii) *piga, cheza, cheka, lima, somo*
(ix) *simu, gazeti, kikokotozi, televisheni, redio*
(x) *bangili, soksi, hereni, mkufu*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 49 26/07/2021 12:02

B. Kuandika wingi wa sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuandika sentensi katika wingi kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa **51** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Wapishi wanapika vyakula vya wageni.
(ii) Tumeandika barua za kirafiki.
(iii) Wanafunzi walisoma vitabu vya hadithi.
(iv) Wanakijiji wamejenga madarasa ya kusomea.
(v) Madaktari watakuwa wanawatibu wagonjwa.
(vi) Wafanyakazi walikuwa wanadai mishahara yao.
(vii) Tuliwauliza walimu kuhusu ufaulu.
(viii) Walimu walituandalia ziara.
(ix) Shule zitafunguliwa kesho asubuhi.
(x) Sisi tunapenda kusoma magazeti.

C. Kujaza chemshabongo kwa kutumia maelezo ya kwenda chini na kwenda kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa **52 - 53** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu fumbo hilo kwa kutumia mfano wa kwenda kulia wa swali la kwanza kwa kuuliza swali lifuatalo:
1. Hali ya kuwa na ghasia (herufi 4) - FUJO

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 50 26/07/2021 12:02

(iv) Andika jibu hilo kwenye vyumba vya kuanzia namba 1 kwenda kulia. Kila chumba kiandikwe herufi moja tu. Tumia herufi kubwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa **52 - 53** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

[1]F	[2]U	[3]J	[4]O					[5]S
[6]U	M	U	A			[7]O	[8]D	A
[9]M	B	A				[10]F	U	A
B	A				[11]K	A	A	
U		[12]O	[13]T	A				
[14]A	[15]N	Z	A					
	[16]Z	A	A					
	I							

D. Kuoanisha maneno yanayokaribiana kimaana kutoka Safu A na Safu B

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutumia mifano ya maneno yanayokaribiana kimaana yaliyopo katika safu A na safu B.

Mfano:

Safu A	Safu B
abiria	msafiri

Katika mfano huo, maana ya neno abiria imeoneshwa katika safu B

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 51 26/07/2021 12:02

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 D ukurasa wa **53** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Zingatia: Mwanafunzi atakayeandika ama herufi ya jibu au neno linalosimama badala ya herufi, wote watakuwa wamepata.

Majibu:

(i)	*f*	*(ix)*	*g*
(ii)	*e*	*(x)*	*j*
(iii)	*a*	*(xi)*	*h*
(iv)	*i*	*(xii)*	*m*
(v)	*d*	*(xiii)*	*n*
(vi)	*b*	*(xiv)*	*c*
(vii)	*p*	*(xv)*	*o*
(viii)	*k*	*(xvi)*	*l*

E. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila kinyume chake.

Mfano: *kumbuka* _____

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.

Mfano: *Kumbuka - sahau*

(iii) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi. Angalia usahihi wa majibu hayo.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 E lililopo ukurasa wa **53** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 52 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*ezua*	*(vi)*	*amani*
(ii)	*tawanya*	*(vii)*	*njaa*
(iii)	*chomoa*	*(viii)*	*tamu*
(iv)	*epua, ipua*	*(ix)*	*funua*
(v)	*mvulana*	*(x)*	*anua*

F. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 6 F ukurasa wa **54** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

Mfano: Walimu wetu ni wakali sana.

Walimu wetu si wakali sana.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 F lililopo ukurasa wa **54** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Sisi hatukufanya ziara shule ya jirani.*
(ii) *Shule yetu haina maktaba kubwa.*
(iii) *Wanafunzi hawasomi vitabu.*
(iv) *Magafu na Minza hawajadiliani kuhusu umuhimu wa maktaba.*
(v) *Mwanafunzi hataandika barua ya kuomba ruhusa.*
(vi) *Shule ya Msingi Miti Mirefu haina matokeo mazuri.*
(vii) *Hajauliza swali darasani.*
(viii) *Mama hajanikumbusha kufua nguo zangu.*
(ix) *Hawajasoma vitabu vya hadithi.*
(x) *Mwalimu hajafundisha Kiswahili.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 53 26/07/2021 12:02

Somo la 8: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kuandaa ziara ya kutembelea shule ya jirani.

(b) Zungumza na wanafunzi kuhusu ziara.

(c) Waongoze wanafunzi kuandaa maswali ya kuwaongoza katika ziara.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya ziara.

(e) Ongoza mjadala kuhusu mambo waliyoyaona baada ya ziara.

(f) Waongoze wanafunzi kuandika habari kuhusu mambo waliyojifunza katika ziara.

(g) Sahihisha kazi hiyo kwa kuzingatia nyakati na alama za uandishi pamoja na mantiki.

Somo la 9: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kuandika habari katika mtiririko mzuri. Zingatia kichwa cha habari, utangulizi, kiini na hitimisho.

(b) Waongoze wanafunzi kusimulia mambo waliyoyaona katika ziara.

(c) Waongoze wanafunzi kupendekeza kichwa cha habari kuhusu ziara.

(d) Waongoze wanafunzi kutaja mambo mbalimbali waliyojifunza katika ziara.

(e) Andika ubaoni mambo waliyoyataja wanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 8 lililopo ukurasa wa **54** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 54 26/07/2021 12:02

Sura ya Saba

Mawasiliano ya simu

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza umuhimu wa simu na jinsi ya kutumia simu katika mawasiliano. Pia, atajifunza maadili mema katika kufanya mawasiliano kwa njia ya simu. Atajifunza kuandika ujumbe mfupi wa simu na kuutuma kwa jamaa au rafiki zake.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma mdahalo kuhusu **umuhimu wa matumizi ya simu katika jamii** na kujibu maswali ya ufahamu

(b) kueleza umuhimu wa simu

(c) kuwasiliana kwa kutumia simu

(d) kuandika ujumbe mfupi wa maandishi wa simu

Mahitaji: vitu halisi, vifani, picha (za kawaida na za mguso), chati ya msamiati, kalamu na daftari

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **55** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Waongoze wanafunzi kusoma kimya mdahalo kuhusu **umuhimu wa matumizi ya simu katika jamii**.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma habari iliyopo ukurasa wa **55 - 59** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) *Nani alikuwa anakaribisha pande mbili kuchangia hoja?*

(ii) *Unadhani upande gani umeshinda?Kwa nini?*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 55 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **56** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza ukurasa wa **59** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao wala uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika msamiati uliopo katika zoezi la pili lililopo ukurasa wa **59 - 60** katika kitabu cha mwanafunzi kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.
(b) Fundisha msamiati huo kwa kutumia vitu halisi, maelezo, picha na maigizo.
(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mdomo kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.
(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 56 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **59 - 60** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo ya jinsi ya kutumia miundo katika sentensi.

(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo.

(d) Waongoze wanafunzi kutambua kanuni za miundo:
….. ilimradi ……., vivyo hivyo, ……. kimoyomoyo……, ……. kinagaubaga .....

(e) Toa mifano ya sentensi zenye miundo iliyopo katika zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mdomo kwa kutumia miundo hiyo na andika sentensi walizotunga ubaoni.

(g) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(h) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu methali.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(c) Andika ubaoni methali walizotaja.

(d) Waongoze wanafunzi kumalizia methali kwa kutumia swali la mfano lililopo zoezi la 4 ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **60** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 57 26/07/2021 12:02

Majibu:

1. *huonekana asubuhi/ni zawadi ya msafiri*
2. *usiokuwa na mwenziwe*
3. *ina mchezo wake*
4. *kuliko libasi*
5. *huliwa na mjinga*
6. *Dira ya binadamu*
7. *Kijumba cha ufisadi*
8. *bali tabia*
9. *Fuata hekima*
10. *kuliko ganda tupu*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kupigia mstari neno lenye maana tofauti na mengine

Hatua za ufundishaji

(i) Andika orodha ya maneno ya mfano ubaoni kutoka zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma orodha ya maneno uliyoyaandika.

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja neno lenye maana tofauti kwa kila orodha.

(iv) Waongoze wanafunzi kupigia mstari neno husika.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) maharage, <u>mtama</u>, kunde, mbaazi
(ii) salio, <u>shule</u>, vocha, pesa
(iii) babaika, wasiwasi, dukuduku, <u>kizunguzungu</u>
(iv) juzi, jana, leo, <u>mchana</u>
(v) chumba, stoo, <u>kitanda</u>, sebule
(vi) wali, ubwabwa, pilau, <u>mchele</u>
(vii) kimyakimya, <u>harakaharaka</u>, kimoyomoyo, kisirisiri
(viii) mawimbi, upepo, kimbunga, <u>giza</u>

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 58 26/07/2021 12:02

(ix) choma, bofya, gusa, bonyeza
(x) rukono, simujanja, nukushi, simutamba

B. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika neno moja linalojumuisha maneno yaliyotolewa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Toa mfano kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika orodha ifuatayo:

Mfano: *wali, kande, ugali, nyama* - vyakula

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililoko ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*mawasiliano*	*(vi)*	*masomo*
(ii)	*siku*	*(vii)*	*wanyama*
(iii)	*magonjwa*	*(viii)*	*nafaka*
(iv)	*vitenzi/ vitendo*	*(ix)*	*matunda*
(v)	*simu*	*(x)*	*ndege*

C. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya maswali yenye majibu ya KWELI au SI KWELI.

Mfano: *Jeska ni mwanafunzi mwenye bidii, utii na ucheshi. KWELI*
Baba yake Jeska anafurahia uhodari na uthubutu wa Jeska kufanya mambo. SI KWELI

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **61** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 59 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*SI KWELI*	(vi)	*KWELI*
(ii)	*KWELI*	(vii)	*KWELI*
(iii)	*SI KWELI*	(viii)	*KWELI*
(iv)	*SI KWELI*	(ix)	*KWELI*
(v)	*SI KWELI*	(x)	*KWELI*

D. Kutunga sentensi sahihi kumi (10) kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita jedwali lililopo zoezi la 5 D ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yaliyomo kwenye jedwali.

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kutoka kwenye jedwali kwa mazungumzo.

(iv) Andika ubaoni sentensi zilizotungwa.

(v) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(vi) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo kwa sauti.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

E. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kukanusha sentensi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 5 E ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine zaidi.

Mfano: *Tutatoka hapa saa sita.*
Hatutatoka hapa saa sita.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 60 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) *Sisi hatukuimba wimbo wa shule.*
(ii) *Siendi kucheza.*
(iii) *Jua halina faida moja tu kwa viumbe hai.*
(iv) *Baba hana duka la simu.*
(v) *Mdogo wangu si mwanafunzi wa Darasa la Pili.*
(vi) *Bahati hatanunua simu.*
(vii) *Watu hawakumiminika kwenye sherehe.*
(viii) *Mwalimu wetu hana simu ndogo.*
(ix) *Kaka haitwi Bahati.*
(x) *Kulwa hajui kupiga simu.*

F. Kuandika sentensi katika wingi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.
(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza wanafunzi dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **62** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) *Tunasoma Shule ya Msingi Tumaini.*
(ii) *Sisi ni wazalendo kwelikweli.*
(iii) *Simu zangu zimepotea leo asubuhi wakati tunachota maji.*
(iv) *Walimu wana simu kubwa zenye rangi nyeupe na nyeusi.*
(v) *Wanaandika ujumbe mfupi wa simu.*
(vi) *Kaka zangu wamenipigia simu.*
(vii) *Watoto wanajua kucheza mipira.*
(viii) *Kakakuona ni wanyama wa ajabu.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 61 26/07/2021 12:02

(ix) *Ng'ombe wamekamuliwa maziwa.*

(x) *Wao watanunua matunda.*

G. Kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi.

Mfano: *Mama_____ ugali. (anapenda, anapendwa, anapendeka)*

Mama <u>anapenda</u> ugali.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **63** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*anazungumza*	*(vi)*	*atakuja*
(ii)	*akiwaletea*	*(vii)*	*anafundisha*
(iii)	*anajua*	*(viii)*	*kumepandwa*
(iv)	*ni*	*(ix)*	*ndiye*
(v)	*si*	*(x)*	*alitufundisha*

H. Kuoanisha maneno ya safu A kwa kuandika maelezo ya safu B ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(a) Andika ubaoni maneno yafuatayo: *simu, simujanja, teknolojia, kompyuta, sebule, mahiri* na *kimoyomoyo.* Wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.

(b) Fundisha maneno hayo kwa kutumia vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 62 26/07/2021 12:02

(c) Waongoze wanafunzi kuoanisha maneno na maana zake kwenye zoezi la 5 H lililoko ukurasa wa **64** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(d) Waongoze wanafunzi wasome maneno na maana zake.
(e) Angalia usahihi wa maneno na maana zake.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 H lililopo ukurasa wa **64** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha kama msamiati na maana zake ziko sahihi.

Majibu:

(i) *Sauti za kubuni na zenye maana zitumiwazo na binadamu ka tika mawasiliano*
(ii) *Kituo maalumu na rasmi kinachojihusisha na shughuli za ki jamii au kiserikali*
(iii) *Kifaa kitumiwacho na watu walioko kwenye maeneo tofauti kupashana habari papo kwa papo*
(iv) *Nasaha au mafunzo anayopewa mtu*
(v) *Simumtelezo*
(vi) *Kiwango cha juu cha uvumbuzi wa kisayansi*
(vii) *Kifaa maalumu kitumikacho kuchapa barua na kuhifadhi kumbukumbu mbalimbali kwenye nakala laini*
(viii) *Chumba maalumu cha kupumzikia ndani ya nyumba*
(ix) *Ujuzi mkubwa wa kufanya jambo fulani*
(x) *Kwa kuongea na nafsi yako bila kutoa sauti*

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu kanuni na utaratibu wa uandishi wa ujumbe mfupi wa simu.
(b) Andika mada uliyoichagua kuiandikia ujumbe wa simu. Tumia mfano uliopo ukurasa wa **64** katika kitabu cha mwanafunzi.

Mfano: salamu kwa baba

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 63 26/07/2021 12:02

(c) Waongoze wanafunzi kuandika ujumbe mfupi wenye maneno yasiyozidi kumi na matano. Waeleze wanafunzi kuwa mtuma ujumbe ataandika jina lake iwapo atatumia simu ya mtu mwingine kutuma ujumbe au mtumiwa hana namba ya simu ya mtumaji. **Mfano:** *Shangazi, napenda kukufahamisha mimi ni mzima wa afya. Msalimie mjomba. Emanueli*.

(d) Wasomee wanafunzi ujumbe huo mfupi au uandike ubaoni ujumbe huo na umchague mwanafunzi mmoja ausome kwa sauti.

(e) Sisitiza maelezo jinsi barua ya kikazi inavyoandikwa na kujibiwa kimaandishi. Toa maelezo ya kina kuhusu kumbukumbu namba inavyoandikwa kwenye barua ya kikazi.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A na B lililoko ukurasa wa **64 - 65** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(g) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, ufupi wa ujumbe na mantiki, mtiririko wa wazo, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya herufi kubwa na idadi ya maneno kwa kuzingatia maelekezo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 64 26/07/2021 12:02

Sura ya Nane

Aina za maneno

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza aina nane za maneno yaani nomino (N), kivumishi (V), kielezi (E), kitenzi (T), kiwakilishi (W), kiunganishi (U), kihusishi (H) , kihisishi (Hs) au kiingizi (I). Vilevile, mwanafunzi atapaswa kubainisha aina hizo za maneno zikiwa katika sentensi mbalimbali kwa kutumia vifupisho vya aina hizo. Somo hili litamsaidia mwanafunzi kutumia aina hizo za maneno kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma ngonjera inayohusu **aina za maneno**
(b) kutamba ngonjera kwa sauti ya utambaji
(c) kubaini wahusika waliopo katika ngonjera
(d) kubaini aina za maneno zilizofafanuliwa katika ngonjera

Mahitaji: vitu halisi, picha, vitendo, bangokitita na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **66** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya ngonjera kuhusu aina za maneno iliyopo ukurasa wa **66 - 69** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu swali lifuatalo:
    (i) Ngonjera uliyoisoma inahusu nini?
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 65 26/07/2021 12:02

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu ngonjera ya **Aina za maneno**. Wakumbushe wanafunzi kanuni na utaratibu wa kusoma ngonjera kwa sauti.

(b) Chagua wahusika Kaka na Dada na kuwapa uhusika katika kusoma ngonjera. Kumbuka kuzingatia jinsi zao.

(c) Toa muda mfupi kwa kila mhusika kusoma sehemu yake.

(d) Waongoze wanafunzi wasome ngonjera kwa kuzingatia uhusika na kanuni za kusoma kwa sauti. Wanaweza kusoma ngonjera hii zaidi ya mara moja kwa kubadili wahusika.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera kwa usahihi. Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wagawe wanafunzi katika makundi mawili, yaani upande wa kaka na upande wa dada, ili wanafunzi wengi waweze kusoma.

(h) Wanafunzi warudie kutamba ngonjera kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika msamiati ufuatao ubaoni: *nomino, kivumishi, kielezi, kitenzi, kiwakilishi, kihisishi, kihusishi na kiunganishi,* kisha wanafunzi wasome na kueleza maana ya kila neno.

(b) Fundisha msamiati huo kwa kutumia vitu halisi, maelezo, picha na maigizo.

(c) Waongoze wanafunzi kutaja maneno mawilimawili kwa kila aina ya maneno. Rekebisha makosa yatakayojitokeza na yaandike maneno hayo ubaoni.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 66 26/07/2021 12:02

hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

Mfano: *Nomino: Zamoyoni* na *mashindano*

Zamoyoni anashiriki mashindano ya mbio.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuoanisha sehemu A na sehemu B ili kuleta maana

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita jedwali lililopo katika zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja maneno yote yaliyopo kwenye sehemu A na sehemu B.

(iii) Waongoze wanafunzi kujibu swali la kwanza kama mfano. Rekebisha papo hapo dosari inapojitokeza.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **70** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) b	*(iii) a*	*(v) d*	*(vii) c*
(ii) f	*(iv) h*	*(vi) e*	*(viii) g*

B. Kujaza fumbo kwa kutumia maelekezo ya kwenda chini na kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita, kama yalivyo katika zoezi la 3 B lililopo kwenye ukurasa wa **71** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Toa mfano wa kwenda kulia wa swali la kwanza kwa

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 67 26/07/2021 12:02

kuuliza swali lifuatalo: *11. Neno linalokaa badala ya nomino (herufi 11) - KIWAKILISHI*

(iii) Andika jibu hilo kwenye vyumba kuanzia namba 11 kwenda kulia. Kila chumba kiandikwe herufi moja. Tumia herufi kubwa.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **71** katika kitabu cha mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

[1]K	I	T	E	[2]N	Z	[3]I			[4]U		
I				O		S			N		
[5]V	U	A		M		H			G		
U			[6]A	I	N	I	[7]S	H	A		[8]K
M				N			I		N		I
I		[9]K	I	O	O		F		I		H
S		I					A		S		I
H		E							H		S
I		[10]L	E	T	A				A		I
		E									S
		Z									H
	[11]K	I	W	A	K	I	L	I	S	H	I

C. Kubainisha nomino zilizotumika katika sentensi kwa kuzipigia mstari

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **72** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zote kumi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C ukurasa wa **72** katika

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 68 26/07/2021 12:02

Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Darasa lina wanafunzi wengi.*
(ii) *Asante sana Yumilia.*
(iii) *Bustani ina matunda mengi sana.*
(iv) *Dada anasoma kitabu chake.*
(v) *Maendeleo ni muhimu kijijini kwetu.*
(vi) *Alikula kwa sababu alikuwa na njaa.*
(vii) *Fundi amekuja na msumeno.*
(viii) *Amepoteza kalamu na rula.*
(ix) *Jeshi lao limeshinda vita.*
(x) *Babu yake ana huruma sana.*

D. Kupigia mstari viwakilishi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za viwakilishi. Waeleze wanafunzi kuwa viwakilishi ni maneno yanayokaa badala ya nomino. Pia, viwakilishi vimegawanyika katika aina nne kama ifuatavyo:

- **Viwakilishi vya nafsi:** kwa mfano *mimi, sisi, wewe, nyinyi, yeye* na *wao*
- **Viwakilishi viulizi:** kwa mfano *vingapi, yupi, wapi* na *lipi*
- **Viwakilishi vioneshi:** kwa mfano *yule, wale, kile, pale* na *ile*
- **Viwakilishi vimilikishi:** kwa mfano *chetu, chao, changu, chake* na *yake*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **72** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 69 26/07/2021 12:02

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **72** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Sisi hatuwajui wao.
(ii) Pale panafahamika sana.
(iii) Ninyi mnafanya nini hapa?
(iv) Wao walihudhuria mkutano ule.
(v) Yupi ameondoka?
(vi) Wawili waende wakachote maji.
(vii) Ambaye amemaliza aje.
(viii) Yale yameharibika sana.
(ix) Chake kimepotea.
(x) Wengine wakae hapa.

E. Kupigia mstari vivumishi katika sentensi
Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za vivumishi. Kumbuka vivumishi vinatoa sifa ya nomino au viwakilishi. Waelekeze kuwa wanapotaja nomino au kiwakilishi wajiulize maswali kama vile yupi, kipi, upi, ipi, yapi na lipi. Jibu watakalopata katika maswali hayo ndilo kivumishi. Kwa mfano, mtoto *yupi*? Jibu lake ni mtoto *mrefu* au mtoto *mnene* nakadhalika. Maneno *mrefu* na *mnene* ndiyo vivumishi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **72** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **72 - 73** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Vijana wengi wana tabia nzuri.
(ii) Panya mkubwa ameingia shimoni.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 70 26/07/2021 12:02

(iii) Kijiji chetu kina zahanati nzuri.
(iv) Amekula chakula chote.
(v) Yeye mwenyewe amefika.
(vi) Wanafunzi wengine watoke nje.
(vii) Mwanafunzi hodari amepata zawadi.
(viii) Maendeleo yetu yanakua kwa kasi.
(ix) Kanga wawili wameatamia.
(x) Mkutano huu umeitishwa na kiongozi wetu.

F. Kubainisha vitenzi katika sentensi kwa kuvipigia mstari

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za vitenzi. Kumbuka kitenzi ni neno linalotoa taarifa kuhusu tendo katika sentensi. Kuna aina tatu za vitenzi ambavyo ni vitenzi vikuu (T), visaidizi (Ts) na vishirikishi (t).

Mfano: Kulwa ameshika tama.
T
Neema alikuwa akikimbia.
Ts T
Yeye si mwema.
t

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **73** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Maswali yafuatayo yatakuongoza kutambua vitenzi. Unafanya nini?, Wanafanya nini? Jibu utakalolipata ndilo kitenzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **73** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Dada na kaka wanatamba ngonjera.
(ii) Kaka anamuuliza dada maswali.
(iii) Dada anamjibu kaka maswali.
(iv) Wezi walivunja duka letu.
(v) Popo si ndege.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 71 26/07/2021 12:02

(vi) Vijana wamebomoa ukuta wote.
(vii) Fundi alitaka kujenga ukuta huo.
(viii) Mvua ilinyesha usiku mzima.
(i) Hii ndiyo nyumba yangu.
(ii) Alicheza na kuimba vizuri.

G. Kupigia mstari vielezi katika sentensi
Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina mbalimbali za vielezi. Kumbuka vielezi hutoa maelezo au taarifa zaidi kuhusu kitenzi. Maswali yafuatayo yatakuongoza kutambua vielezi. Unatanguliza kitenzi na kuongeza maneno wapi au nini. Jibu utakalolipata ndilo kielezi. Kwa mfano, *Swali:Unakwenda wapi? Jibu: Ninakwenda shuleni. Shuleni ni kielezi.*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo katika zoezi la 3 G ukurasa wa **73** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **73** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Maji yamejaa pomoni.
(ii) Kaa anakwenda upandeupande.
(iii) Pikipiki ilitumbukia bwawani taratibu.
(iv) Daktari atafika keshokutwa.
(v) Ataondoka mapema ili kuwahi usafiri.
(vi) Mwanafunzi anatembea polepole.
(vii) Walimpiga sana.
(viii) Alihesabu vizuri ili kupata jibu.
(ix) Humtembelea kila siku.
(x) Simba ananguruma sana.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 72 26/07/2021 12:02

H. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia vihisishi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja vihisishi mbalimbali. Kumbuka vihisishi ni maneno yanayoonesha hisia ya mzungumzaji kama vile huzuni, furaha, mshangao nakadhalika. Pia, mwisho huwekwa alama ya mshangao.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 H ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo kwenye ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Majibu ya zoezi hili yatategemeana na majibu ya wanafunzi.

I. Kubainisha aina za maneno katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja vifupi vya aina za maneno na uviandike ubaoni. Wakati wanafunzi wanataja vifupi hivyo baini dosari na uzirekebishe papo kwa hapo.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo kumi kwa sauti.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 I ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 I lililopo ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) Juma alinunua sabuni yake.
N T N V

(ii) Katundu alijipaka mafuta mazuri.
N T N V

(iii) Sote tunatunga sentensi sahihi.
W T N V

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 73 26/07/2021 12:02

(iv) Mmoja atakuja mapema.
W T E

(v) Aah! Wewe angalia usinase.
H W Ts T

(vi) Sisi tulisikitika goli lile lilipoingia wavuni.
W T N V T E

(vii) Mahakama yetu inatoa huduma bora.
N V T N V

(viii) Paka shume aliingia bandani kukamata kuku.
N V T E T N

(ix) Aisee! Twende tukalale nimechoka.
H Ts Ts T

(x) Uji ulimwagika mwaa!
N T E

(xi) Baba ndiye mwalimu mkuu.
N t N V

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujadili mambo wanayoyapenda na uyaandike ubaoni.

(b) Toa maelezo jinsi ya kutunga hadithi yoyote anayoipenda yenye maneno yasiyozidi mia moja ishirini (120), kisha apigie mstari nomino na vitenzi. Kumbuka kila mstari mmoja hukadiriwa kuwa na maneno kumi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **74** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa kuandika kwenye madaftari yao.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, nomino na vitenzi, idadi ya maneno na mwandiko safi. Baada ya kusahihisha, chagua kazi iliyoandikwa vizuri wanafunzi waisome darasani kwa sauti.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 74 26/07/2021 12:02

Sura ya Tisa

Risala

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma na kuandika risala kwa kuzingatia muundo wa risala. Pia, atajifunza kuandika risala. Vilevile, ataimba wimbo unaohusu Mwenge wa Uhuru na kufanya mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma na kuandika risala
(b) kuimba wimbo unaohusu Mwenge wa Uhuru
(c) kueleza umuhimu wa Mwenge wa Uhuru

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), kalamu rashasha, bangokitita na karatasi ngumu (manila)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo kwenye kipengele cha *fikiri* kilichopo ukurasa wa **75** katika Kitabu cha Mwanafunzi ili kukuza stadi ya kuzungumza na kusikiliza. Pia, kufahamu uelewa wa mwanafunzi katika somo hili.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya Mwenge wa Uhuru iliyopo ukurasa wa **75 - 79** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Habari uliyoisoma inahusu nini?
    (ii) Wanafunzi wa Shule ya Msingi Changanyikeni waliimba wimbo gani?
    (iii) Wimbo huo ulikuwa na ujumbe gani?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 75 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa kifupi.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **79** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kifanyike katika somo hili.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda kisha rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *wadia, kifunguakinywa, jiwe la msingi, shamrashamra, kandokando, punga, shauku, fursa, shuhudia, bashasha, wasaa, msafara, risala* na *miundombinu* kwa kutumia maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.
(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 76 26/07/2021 12:02

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.
(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa kama mfano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja nyakati mbalimbali.
Mfano: *wakati uliopo na ujao*
(ii) Kumbuka kuwa, silabi inayoonesha wakati uliopita katika kitenzi ni *li*
(iii) Andika ubaoni sentensi zilizopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iv) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizoandikwa ubaoni.
(v) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopita.Tumia mifano iliyopo zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

B. Kuandika vinyume vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Toa mifano ya vinyume vya maneno kama ilivyooneshwa kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **80** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 77 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*huzuni*	*(v)*	*giza*	*(viii)*	*bonde*
(ii)	*taabu*	*(vi)*	*upole*	*(ix)*	*hasara*
(iii)	*laana*	*(vii)*	*chuki*	*(x)*	*mwovu*
(iv)	*mwanafunzi*				

C. Kuandika neno moja lenye maana sawa na tungo zilizoorodheshwa, kisha kutunga sentensi moja kwa kila neno.

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizo katika zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **81** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 3 C ukurasa wa **81** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Andika ubaoni neno ulilolipata katika sentensi ya kwanza, kisha tunga sentensi kwa kutumia neno hilo.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **81** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *dhulumu*
(ii) *bashiri / tabiri*
(iii) *safiri*
(iv) *bungeni*
(v) *chuna*
(vi) *kumbuka*
(vii) *zawadi*
(viii) *shangaa, ajabia, duwaa, tunduwaa*

D. Kutunga maswali kumi (10) sahihi kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 78 26/07/2021 12:02

(ii) Chora ubaoni jedwali lililopo ukurasa wa **81** katika Kitabu cha Mwanafunzi

(iii) Waongoze wanafunzi kusoma safu ya kwanza, ya pili na ya tatu.

(iv) Toa mfano mmoja wa swali kutokana na jedwali.

(v) Waongoze wanafunzi kutunga maswali kwa usahihi kwa kutumia jedwali kwa njia ya mazungumzo.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **81** katika Kitabu cha Mwanafunzi katika madaftari yao.

(vii) Kagua usahihi wa maswali yaliyotungwa na wanafunzi.

E. Kupanga sentensi ili zilete mtiririko sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo zoezi la 3 E ukurasa wa **81 - 82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waulize wanafunzi kama wamegundua kosa lolote wakati wanasoma sentensi hizo.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **81 - 82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*ix*	(iv)	*v*	(vii)	*x*	(ix)	*vi*
(ii)	*iii*	(v)	*ii*	(viii)	*iv*	(x)	*vii*
(iii)	*i*	(vi)	*viii*				

F. Kuandika maneno mengine yenye maana zinazofanana na maneno yaliyotajwa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 3 F ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuonesha maneno mengine yanayofanana kimaana.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 79 26/07/2021 12:02

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *munyu*
(ii) *divai*
(iii) *alfajiri, macheo, mapambazuko*
(iv) *zaidi, tele, pomoni*
(v) *majonzi, simanzi, sikitiko*
(vi) *waraka*
(vii) *faragha, fumbo*
(viii) *bilauri*
(ix) *kigoli, mwanamwali, binti*
(x) *ghulamu, barobaro, mvuli, kijana, shababi*
(xi) *mwamba, jiwe*
(xii) *nuru*

G. Kuandika KWELI au SI KWELI

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutoa mfano wa sentensi za kujibu KWELI au SI KWELI. Unaweza kutumia sentensi ya kwanza au ya pili kama mfano katika zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **82** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Ongeza sentensi nyingine ili kujenga umahiri katika zoezi hili.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **82 - 83** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *KWELI*
(ii) *SI KWELI*
(iii) *KWELI*
(iv) *SI KWELI*
(v) *SI KWELI*
(vi) *KWELI*
(vii) *KWELI*
(viii) *KWELI*
(ix) *SI KWELI*
(x) *KWELI*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 80 26/07/2021 12:02

H. Kupigia mstari neno lisiloendana na maneno mengine katika kila kifungu cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno ya swali la (i) hadi la (x) katika zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **83** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi hili kuonesha jinsi ya kupigia mstari neno lisilohusika.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **83** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*shule*	*(iv)*	*duara*	*(vii)*	*nyumba*
(ii)	*rambirambi*	*(v)*	*waridi*	*(viii)*	*ndoo*
(iii)	*fadhaa*	*(vi)*	*mwenge*	*(ix)*	*posta*

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Ongoza majadiliano kuhusu risala, muundo wa risala na namna ya kuandika risala.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **83** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi na mtiririko wa mawazo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 81 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi

Kutumia kamusi

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza maana ya kamusi na jinsi ya kuitumia. Vilevile, atajifunza msamiati, nahau, methali, uundaji wa maneno, utungaji na mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari kuhusu **Ugonjwa wa maana**
(b) kubaini maana ya kamusi
(c) kutaja vitu vya msingi katika kuitumia kamusi
(d) kubaini namna ya kuitumia kamusi

Mahitaji: kamusi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya methali, bangokitita, kalamu rashasha, chati ya nahau na chati ya alama za uandishi

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **84** katika Kitabu cha Mwanafunzi ili kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza.
(b) Tumia picha iliyopo katika ukurasa wa **86** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Ugonjwa wa maana.**
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Ugonjwa wa maana** iliyopo katika ukurasa wa **84 - 87** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole na bila kutoa sauti.
(d) Waulize maswali yafuatayo:

(i) Unafikiri mgonjwa angeweza kutibiwa na daktari mwingine?
(ii) Kama ndiyo, taja jina la daktari huyo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 82 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyosoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi, kufanya zoezi la kwanza la ufahamu lililopo ukurasa wa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari itakayosomwa.
(b) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili ili kuonesha mfano mzuri wa usomaji, kwa kuzingatia kanuni sahihi za usomaji.
(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsi zao na kiwango cha usomaji. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, fuatilia usomaji ili ubaini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda ili kurekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *kidahizo, maarifa, kitomeo, tafsiri, maana, kamusi, maneno, lugha, msamiati, alfabeti, herufi, taarifa* na *matamshi* kwa kutumia maelezo, matendo, mazingira halisi na picha.
(b) Andika maneno hayo ubaoni, na wanafunzi wayasome.
(c) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yanayofanana kwa kila neno walilopewa.
(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 83 26/07/2021 12:02

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi, kisha watunge sentensi nyingine kwa kuandika.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **87** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasirudie sentensi zilizotungwa wakati wa somo.

Somo la 4: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo hili. Sisitiza waandike imla hiyo kwa hati ya wima ya kuunga. Pia, wazingatie alama za uandishi.
(b) Wasomee wanafunzi imla ifuatayo kwa kasi ya kawaida. Wanafunzi wasikilize bila kuandika.

> *Kamusi ni kitabu kilichopanga maneno kialfabeti na kutoa maana zake. Pia, kinabainisha aina za maneno na kuonesha matamshi sahihi ya maneno. Vilevile, kinaonesha wingi na umoja pamoja na mifano ya matumizi ya maneno hayo.*

(c) Wasomee tena mara ya pili kwa kufuata vituo na alama za uandishi huku wakiandika kwenye madaftari yao.
(d) Wasomee taratibu huku wao wakifuatisha na kuhakiki kile walichokiandika.
(e) Sahihisha kazi kwa kuzingatia uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, matumizi ya alama za uandishi, matumizi ya herufi kubwa, hati ya wima ya kuunga na usafi.

Somo la 5: Nahau na Misemo

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja misemo mbalimbali wanayoifahamu.
(b) Waongoze wanafunzi kufafanua na kutoa maana ya misemo.

Mfano: *piga kituo - pumzika katika kazi fulani*

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **87 - 89** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 84 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*gugumiza maneno*	*(vi)*	*kuwa na mkono mzito*
(ii)	*gwaya moyo*	*(vii)*	*macho makavu*
(iii)	*iva macho*	*(viii)*	*pata mwili*
(iv)	*kata hukumu*	*(ix)*	*weka muhula*
(v)	*kufa mbavu*	*(x)*	*weka msingi*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuoanisha maneno kutoka safu A na vinyume vyake kutoka safu B

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili zoezi hili ubaoni au wanafunzi wafungue ukurasa wa **89** kwenye vitabu vyao.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno yote kwenye zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Sisitiza kuanza na safu A kisha safu B

(iii) Hakikisha kila mwanafunzi anasoma kwa sauti.

(iv) Wakati wanafunzi wanasoma, fuatilia usomaji ili ubaini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo.

(v) Toa mifano michache ya jinsi ya kuoanisha safu hizi mbili.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu :

(i)	*f*	*(iv)*	*c*	*(vii)*	*i*	*(ix)*	*j*
(ii)	*g*	*(v)*	*d*	*(viii)*	*b*	*(x)*	*h*
(iii)	*e*	*(vi)*	*a*				

B. Kubadili sentensi kuwa katika hali ya mazoea

(i) Toa maelezo kuhusu hali ya mazoea katika sentensi. Hali ya mazoea huoneshwa na silabi *hu-* katika kitenzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 85 26/07/2021 12:02

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 B lililopo kwenye ukurasa wa **89** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **89 - 90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

C. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za kufundisha

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 C lililopo kwenye ukurasa wa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) karai (iv) garimoshi (vii) harakaharaka (ix) soko
(ii) munyu (v) motokaa (viii) kokoto (x) mkeka
(iii) tasa (vi) neno

D. Kupanga maneno kialfabeti

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja mpangilio wa alfabeti kuanzia A - Z.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*alfabeti*	*(vii)*	*kikombe*	*(xiii)*	*mwalimu*
(ii)	*dada*	*(viii)*	*kituo*	*(xiv)*	*ndoo*
(iii)	*herufi*	*(ix)*	*mama*	*(xv)*	*nguo*
(iv)	*Januari*	*(x)*	*maneno*	*(xvi)*	*polisi*
(v)	*kataza*	*(xi)*	*miti*	*(xvii)*	*sahani*
(vi)	*kijiji*	*(xii)*	*mtu*	*(xviii)*	*shule*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 86 26/07/2021 12:02

E. Kutunga sentensi kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita zoezi la 4 E lililopo ukurasa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia jedwali kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 4 E ukurasa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kutoka kwenye jedwali kwa mazungumzo.

(iv) Andika ubaoni sentensi zilizotungwa.

(v) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa **90** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

F. Kuandika maneno kumi na matano kutokana na jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Chora jedwali lililopo katika zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **91** katika Kitabu cha Mwanafunzi ubaoni au kwenye bangokitita.

(ii) Toa mfano mmoja uliozungushiwa ukurasa wa **91** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **91** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

alfabeti, beti, neno, noti, neti, yowe, kitoweo, kibuyu, kito, doa, kambo, safu, kutu, zetu, kaka, aibu, wakili, oa, bei, amka, uso (majibu itategemeana na majibu ya mwanafunzi).

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 87 26/07/2021 12:02

G. Kuzungushia herufi ya jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 G lililopo kwenye ukurasa wa **91 - 92** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(ii) Waongoze wanafunzi kutumia penseli kuzungushia majibu sahihi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **91 - 92** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) c (iii) a (v) a (vii) c (ix) d
(ii) d (iv) d (vi) b (viii) c (x) c

H. Kutunga sentensi mbili zenye maana tofauti kwa kila neno

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili maneno yote yaliyopo kwenye zoezi la 4 H ukurasa wa **92** kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kuyasoma maneno hayo kwa sauti na kwa usahihi.

(iii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo.

(iv) Andika sentensi hizo ubaoni. Angalia usahihi wa sentensi wanazozitunga wanafunzi.

(v) Rekebisha makosa papo hapo pale yanapojitokeza.

(vi) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **92** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(vii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **92** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha hawarudii sentensi walizotunga wakati wa somo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 88 26/07/2021 12:02

Somo la 7: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Gawa kamusi kwa wanafunzi. Mgao utategemea idadi ya wanafunzi wako darasani na kamusi zilizopo.

(b) Waongoze wanafunzi kukumbuka maana ya kidahizo na kitomeo kwa kuwauliza maswali.

(c) Andika majibu yote ya wanafunzi ubaoni.

(d) Wakati wanafunzi wanajibu, rekebisha dosari zinazojitokeza.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **92** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(f) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa kidahizo na kitomeo chake, alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **92** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **92** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia neno na maana yake, mpangilio wa kialfabeti, aina ya ngeli na alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo, matumizi ya herufi kubwa na idadi ya maneno.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 89 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Moja

Matangazo ya biashara

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu mambo ya kuzingatia katika uandishi wa matangazo ya biashara. Atajifunza kuandika matangazo ya biashara. Pia, atasoma habari na kujibu maswali. Vilevile, atajifunza msamiati, muundo wa matangazo ya biashara, mazoezi mbalimbali ya lugha, utungaji pamoja na kazi ya kufanya.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari kuhusu **Nkosi asoma tangazo la biashara**
(b) kueleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa matangazo ya biashara
(c) kuandika matangazo mbalimbali ya biashara

Mahitaji: vitu halisi, chati za matangazo, kalamu rashasha, matangazo mbalimbali ya biashara, kadi za maneno, kadi za sentensi, picha mguso, bangokitita na diski ya matangazo

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa wa **93** kwenye kipengele cha *fikiri* katika kitabu cha mwanafunzi.
(a) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Nkosi asoma tangazo la biashara** iliyopo katika ukurasa wa **93 - 96** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha vidole wala kutoa sauti.
(b) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Taja aina ya tangazo ulilolisoma katika habari.
    (ii) Tangazo hilo linahusu nini?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 90 26/07/2021 12:02

(c) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **96** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza nini unatarajia kufanya katika somo hili.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *tangazo, biashara, mawasiliano, taarifa, habari, mtandao, intaneti, teknolojia, tovuti,* nukushi, *baruapepe* na *hifadhi* kwa kutumia mbinu za maelezo, vitu halisi, picha na maigizo.
(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.
(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.
(d) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 91 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili ukurasa wa **97** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Methali

Hatua za Ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.

(b) Toa mfano uliopo zoezi la 3 ukurasa **97** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **97** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

1. *husingizia jua*
2. *Mgagaa na upwa*
3. *furaha ya mvuvi*
4. *Dunia hadaa*
5. *hakina rubani*
6. *Msema kweli*
7. *Ulimi unauma*
8. *si hoja*
9. *Vita vya panzi*
10. *haiamuliwi kwa fimbo*

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kutumia herufi za maneno uliyopewa kuunda maneno mengine mapya

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kuunda maneno mengine kutokana na herufi za maneno waliyopewa. Tumia mifano ifuatayo:

Lima - mali

Paka - kapa

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 92 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*oka*	*(ii)*	*oza, zao*	*(iii)*	*bao*
(iv)	*kata*	*(v)*	*zako*	*(vi)*	*lami*
(vii)	*leo*	*(viii)*	*wape / pawe*	*(ix)*	*wale*
(x)	*akiba*				

B. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu kinyume cha maneno.

(ii) Waongoze wanafunzi kutoa kinyume cha maneno kwa kutumia mfano uliopo kwenye zoezi la 4 B ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B ukurasa wa **98** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*itika*	*(vi)*	*mpumbavu, mjinga*
(ii)	*msichana*	*(vii)*	*mvivu*
(iii)	*mdogo*	*(viii)*	*mtu mzima*
(iv)	*mpole*	*(ix)*	*mwanafunzi*
(v)	*mgeni*	*(x)*	*giza*

C. Kujaza fumbo kwa kutumia maelezo ya kwenda chini na kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili fumbo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **99** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Toa mfano wa kwenda chini wa swali lifuatalo:

1. Mtu anayefundisha (herufi 7) *MWALIMU*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 93 26/07/2021 12:02

(iv) Andika jibu lako kwenye chumba kuanzia namba 1 kwenda chini. Kila chumba kiandikwe herufi moja.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **99** katika Kitabu cha Mwanafunzi katika madaftari yao.

Majibu:

		[2]M							
		B						[5] M	
		U						W	
					[3]U			A	
[1] M	A	[4] A	N	D	A	M	A	N	O
W		D			D			A	
A		H			U			F	
L		A			I			U	
I		B						N	
M		U			[6] M	B	U	Z	I
U								I	

D. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi namna ya kukanusha sentensi kwa kutumia mfano uliopo katika zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **99** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine. Zingatia silabi *ha*, *hu*, na *si* zinaonesha ukanushi kwenye kitenzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 94 26/07/2021 12:02

Mfano: Nkosi alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini.

Nkosi <u>hakuwa</u> kijana mwenye umri wa miaka ishirini.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **99 - 100** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Vijana wengi hawapendi kukaa bila kufanya kazi.

(ii) Nkosi hakuona tangazo kuhusu uuzaji wa kiwanja.

(iii) Maganga hafanyi kazi ya ualimu.

(iv) Tangazo la biashara halijatumia lugha inayoeleweka au Tangazo la biashara limetumia lugha isiyoeleweka.

(v) Maganga hakuona tangazo la biashara Mtaa wa Kijiweni.

(vi) Shuleni si mahali pa kwenda kucheza.

(vii) Mimi sijasoma tangazo la biashara.

(viii) Mwalimu hajafundisha kuhusu uandishi wa matangazo ya biashara.

(ix) Baba hajasoma gazeti leo.

(x) Huwezi kulipia vitabu kwa njia ya nukushi.

E. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 E ukurasa wa **100** katika Kitabu cha Mwanafunzi kueleza dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi zaidi kuhusu wingi na umoja, kwenye zoezi la 4 E lililopo ukurasa 100 katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 95 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i)	*mikoa*	*(v)*	*vyeo*	*(viii)*	*biashara*
(ii)	*jengo*	*(vi)*	*wanunuzi*	*(ix)*	*vijana*
(iii)	*watumishi*	*(vii)*	*tangazo*	*(x)*	*magazeti*
(iv)	*mtaa*				

F. Kamilisha sentensi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo litakalofundishwa.

(ii) Waongoze wanafunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia swali la kwanza kama mfano katika zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **100** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **100 - 101** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Sahihisha kazi za wanafunzi na kufanya marudio pale yanapohitajika.

Majibu:

(i)	*kizuri*	*(iv)*	*vizuri*	*(vii)*	*mzuri*	*(x)*	*vizuri*
(ii)	*nzuri*	*(v)*	*nzuri*	*(viii)*	*wazuri*	*(xi)*	*pazuri*
(iii)	*mzuri*	*(vi)*	*kizuri*	*(ix)*	*nzuri*		

G. Kuoanisha maneno ya sehemu A na maelezo yake kutoka sehemu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi mbele ya maelezo ya sehemu A

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano wa kuoanisha maneno ya sehemu A na B ili sehemu za tangazo la biashara zilandane au zifanane.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 96 26/07/2021 12:02

Mfano:

Sehemu A	Sehemu B
(i) Kichwa cha tangazo C	JIPATIE VITABU KWA BEI NAFUU

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **101** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia sehemu za tangazo la biashara.

Somo la 6: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya, nafasi kati ya neno na neno na matumizi ya herufi kubwa.

(b) Soma kwa makini kifungu cha habari huku wanafunzi wakisikiliza.

Kaka yangu ni mfanyabiashara wa duka la nguo kijijini kwetu. Yeye hutangaza biashara zake kupitia mitandao ya kijamii. Huandika matangazo ya biashara yake ya nguo kwenye simu yake ya mtelezo. Huanza kuandika kichwa cha tangazo. Hukiandika kwa herufi kubwa. Baadaye, huandika aina za nguo anazoziuza na mahali anapouzia. Mwishoni mwa tangazo, huandika mawasiliano yake. Hapo huandika namba ya simu na baruapepe yake. Hatimaye, hutuma katika mitandao ya kijamii. Hufanya hivyo ili kupatikana kwa urahisi pale wateja wake wanapohitaji bidhaa zake. Kutokana na matangazo hayo, kaka ana wateja wengi. Hutuambia kuwa biashara ni matangazo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 97 26/07/2021 12:02

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika kwenye madaftari yao.
(d) Soma kifungu chote ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.
(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa na usafi wa kazi.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo jinsi ya kuandika tangazo la biashara kwa kufuata kanuni na taratibu za uandishi wa tangazo.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia katika uandishi wa matangazo ya biashara.
(c) Andika ubaoni majibu ya wanafunzi na rekebisha papo hapo makosa yanapojitokeza.
(d) Waongoze kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **101** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.
(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko mzuri, nafasi kati ya neno na neno, mambo muhimu katika tangazo na matumizi sahihi ya herufi kubwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 98 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Mbili

Uundaji wa maneno

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza namna ya kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili. Pia, atasoma shairi la **Yai au Kuku (Jibu)** na kujibu maswali. Vilevile, atajifunza misamiati, miundo, mazoezi mbalimbali ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma na kughani shairi la **Yai au Kuku (Jibu)** na kujibu maswali ya ufahamu
(b) kuigiza shairi hilo
(c) kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili
(d) kutunga habari

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya msamiati, kadi za maneno, kalamu rashasha na bangokitita

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **102** katika Kitabu cha Mwanafunzi ili kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza pamoja na kupata uelewa wa mwanzo alionao mwanafunzi kuhusu somo utakalofundisha.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya shairi la **Yai au Kuku (Jibu)** lililopo ukurasa wa **102 - 103** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 99 26/07/2021 12:02

(i) *Hivi unadhani kati ya kuku na yai nani alianza?*

(ii) *Je, kuna umuhimu wa kumheshimu mtu aliyekuzidi umri?*

(d) Waongoze wanafunzi wasimulie shairi walilolisoma kwa maneno machache.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma shairi kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *mzozo, tatua, maelewano, taharuki, ubishi, himahima, ringa, jalala, ufasaha, tabasamu* na *beza* kwa kutumia vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 100 26/07/2021 12:02

(b) Andika maneno hayo ubaoni na uwaongoze wanafunzi kuyasoma.
(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.
(d) Waongoze wanafunzi kubaini maneno *mzozo, maelewano, ubishi, himahima* na *ufasaha* namna yalivyoundwa.
(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia misamiati hiyo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni na angalia usahihi wa sentensi walizozitunga wanafunzi.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 4: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Teua wahusika kwa kuzingatia wahusika waliopo kwenye shairi yaani Yai na Kuku.
(b) Toa maelekezo kwa wahusika.
(c) Wape muda wahusika wajiandae na kuwasilisha kazi yao.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **104** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Fanya hitimisho la igizo na wapongeze wahusika.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika vifupisho vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni mfano wa maneno na vifupisho vyake.

Mfano: *Baraza la Kiswahili la Taifa - BAKITA*

(ii) Tumia mfano uliopo kwenye zoezi la 4 A kuwaongoza wanafunzi kufanya zoezi hili. Katika mfano huo, sisitiza kwamba herufi au silabi za mwanzo wa neno ndizo zinazotumika kuandika vifupisho. Pia, waeleze kuwa vifupisho vya maneno huandikwa kwa herufi kubwa bila nukta.
(iii) Waongoze wanafunzi kuandika vifupisho vya maneno mengine.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 101 26/07/2021 12:02

(iv) Angalia usahihi wa vifupisho hivyo.

(v) Waongoze kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **104 - 105** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) UKIMWI
(ii) TAMISEMI
(iii) JKT
(iv) TAKUKURU
(v) TEHAMA
(vi) MEMKWA
(vii) UMITASHUMTA
(viii) CWT
(ix) TET
(x) CHANETA
(xi) BASATA
(xii) MKUKUTA

B. Kuunda nomino kutokana na vitenzi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu namna ya kuunda nomino kutokana na vitenzi.

(ii) Nakili ubaoni mfano uliopo katika zoezi la 4 B ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja nomino zinazotokana na kitenzi *cheka.*

(iv) Andika nomino hizo ubaoni.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) wimbo, mwimbaji, uimbaji
(ii) somo, kisomo, msomi, usomi, usomaji, msomaji
(iii) shindano, ushindani, mshindi, mshindani
(iv) mwandishi, mwandiko, uandishi, uandikaji
(v) mlevi, kileo, kilevi, ulevi
(vi) burudani, burudiko, mburudishaji, kiburudisho
(vii) mchezo, mchezaji, uchezaji
(viii) mchoro, mchoraji, uchoraji
(ix) kilimo, mkulima, ukulima, ulimaji
(x) kiongozi, mwongozo, uongozi, uongozaji

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 102 26/07/2021 12:02

C. Kuunda maneno mengine kwa kudondosha silabi moja

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno ambayo silabi moja itadondoshwa.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 C ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuunda maneno mengine kwa kudondosha silabi moja.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti maneno mapya yaliyoundwa baada ya kudondosha silabi moja.

Majibu:

(i)	*ndoo/ kondo*	*(vi)*	*lima*
(ii)	*buni*	*(vii)*	*shari*
(iii)	*lewa*	*(viii)*	*mto*
(iv)	*zinga*	*(ix)*	*koa*
(v)	*ziwa*	*(x)*	*kiko, kombe*

D. Kuandika sentensi kwa usahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo kuhusiana na kuandika sentensi kwa usahihi.

(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuandika sentensi kwa usahihi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **105** katika Kitabu cha Mwanafunzi katika madaftari yao.

(iv) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizoandikwa kwa usahihi.

Majibu:

(i) Ng'ombe anakula mahindi shambani.

(ii) Watoto wangu wanacheza nje.

(iii) Unga umemwagika uwanjani.

(iv) Mimi ninakwenda shuleni asubuhi / Mimi huenda shuleni asubuhi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 103 26/07/2021 12:02

(v) Wantiko ni rafiki yangu.
(vi) Tuliposafiri, tulilala siku mbili njiani.
(vii) Aliponea chupuchupu.
(viii) Alikula baadhi ya matunda tu.
(ix) Moto unawaka kwa kasi.
(x) Nilifika jana alasiri.

E. Kuandika maneno kwa kirefu

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(ii) Nakili vifupisho ubaoni.
(iii) Waongoze wanafunzi kusoma vifupisho hivyo kwa sauti.
(iv) Tumia mifano iliyopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:
(i) mama mdogo
(ii) bwana mdogo
(iii) baba yako
(iv) dada yake
(v) Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
(vi) Upungufu wa Kinga Mwilini
(vii) Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
(viii) Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania
(ix) Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania
(x) Baraza la Michezo Tanzania

Somo la 6: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu namna ya kutumia miundo katika sentensi.
(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 5 ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma miundo hiyo ubaoni.
(d) Tumia mifano iliyopo zoezi la 5 ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 104 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia miundo hiyo kwa mazungumzo na andika sentensi hizo ubaoni.
(f) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi katika madaftari yao. Sentensi hizo ziwe tofauti na zile zilizotolewa kwenye mfano.

Somo la 7: Kazi ya kufanya

Hatua za ufundishaji

(a) Andaa maneno ya kutosha yaliyoundwa kwa vifupisho.
(b) Gawa wanafunzi katika makundi kwa kuzingatia jinsi.
(c) Waongoze wanafunzi kuchagua viongozi wa vikundi.
(d) Gawa maswali kwa kila kundi.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo la utungaji.
(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuwaongoza kwa kuwauliza maswali yafuatayo:
    (i) Andika maelezo mafupi juu ya shule yako.
    (ii) Unapenda mchezo gani?
    (iii) Taja michezo mnayocheza hapa shuleni.
    (iv) Michezo hiyo huwa inachezwa wakati gani?
    (v) Taja faida mnazopata kutokana na michezo hiyo.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **106** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.
(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo na matumizi ya herufi kubwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 105 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Tatu

Ufupisho

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma hadithi na kubaini mawazo makuu. Ataandika ufupisho kwa kuzingatia mawazo makuu bila kupotosha maana ya hadithi. Atafanya mazoezi yote yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi
(b) kubaini mawazo muhimu katika hadithi
(c) kubaini na kueleza maana ya maneno katika hadithi
(d) kufupisha hadithi kwa kuisimulia
(e) kuandika ufupisho wa hadithi

Mahitaji: vitu halisi, michoro, picha (za kawaida na mguso), hadithi mbalimbali, manila na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **107** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi kuhusu **Maisha ya kuku** iliyopo ukurasa wa **107 - 109** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasome bila kufuatisha kwa vidole wala kutoa sauti.
(c) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
    (i) Kitu gani kimekuvutia katika hadithi uliyosoma? Kwa nini?
    (ii) Umegundua nini katika hadithi hiyo?
    (iii) Umejifunza nini kutokana na hadithi hiyo?
    (iv) Kwa nini mtunzi anahimiza elimu?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 106 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu lugha ya picha iliyotumika katika hadithi ukurasa wa **108** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi wajadili uhalisia wa hadithi ya **Maisha ya kuku** katika maisha halisi ya binadamu.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **110** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi kanuni na utaratibu sahihi wa kusoma kwa sauti.
(b) Toa maelezo mafupi kuhusu usomaji sahihi wa hadithi kwa kuzingatia alama za uandishi.
(c) Wakumbushe wanafunzi kuhusu usomaji unaozingatia alama za uandishi.
(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, kwa kuzingatia jinsi. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza katika usomaji na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri inavyowezekana.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *dhiyaa, kifani, tawazwa, hodari, ng'ambo, dhamiria, kithiri, utafiti, ajira* na *ngome.* Unaweza kutumia mbinu mbalimbali kama vile maelezo, mjadala, igizo, maswali na majibu.
(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja kama lilivyotumika kwenye habari. Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa mdomo kwa kutumia maneno hayo.
(c) Andika sentensi hizo ubaoni na kuangalia kama ziko sahihi. Washirikishe wazisome kwa sauti.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 107 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **110** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga, hazifanani na zile walizotunga kama mifano wakati wa kipindi.

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu miundo.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma miundo iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **110 - 111** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Tumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 3 kuonesha jinsi ya kutunga sentensi kwa kutumia miundo.

(d) Sahihisha makosa yanayojitokeza katika utunzi wa sentensi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **110 - 111** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kuandika herufi ya jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia swali la kwanza kama mfano kuonesha namna ya kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **111** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **111 - 112** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*a*	*(vi)*	*d*
(ii)	*b*	*(vii)*	*d*
(iii)	*d*	*(viii)*	*d*
(iv)	*a*	*(ix)*	*d*
(v)	*a*	*(x)*	*d*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 108 26/07/2021 12:02

B. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika NDIYO au HAPANA

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo.

(ii) Andika mifano ya maswali ubaoni na uwaongoze wanafunzi wayajibu.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*NDIYO*	*(vi)*	*HAPANA*
(ii)	*NDIYO*	*(vii)*	*HAPANA*
(iii)	*NDIYO*	*(viii)*	*HAPANA*
(iv)	*HAPANA*	*(ix)*	*HAPANA*
(v)	*NDIYO*	*(x)*	*NDIYO*

C. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya kukanusha sentensi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi na uziandike ubaoni.

(iii) Waongoze wanafunzi kukanusha sentensi walizotunga.

(iv) Toa maelezo kuhusu mfano uliopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi ukurasa wa **113**.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **113** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Kuku hawajitambui.

(ii) Maisha ya kuku hayavutii ndege wengine.

(iii) Kuku hawezi kupambana na kicheche.

(iv) Swea si kifaranga mdadisi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 109 26/07/2021 12:02

(v) Koba si kisiwa cha amani.

(vi) Kuku hawana jeshi imara.

(vii) Wakili hakupenda kusoma vitabu na magazeti.

(viii) Vijana hawana umoja.

(ix) Hajajenga kiwanda cha kusindika samaki.

(x) Buibui hatasanifu majengo.

D. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kwa wanafunzi jinsi ya kujaza nafasi wazi.

(b) Waongoze wanafunzi kujaza nafasi wazi kwa kutumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **113 - 114** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*mkato*	*(vi)*	*hadithi*
(ii)	*aya*	*(vii)*	*msamiati*
(iii)	*kufupisha*	*(viii)*	*yamini*
(iv)	*alama ya mshangao*	*(ix)*	*dhiyaa*
(v)	*alama ya kuuliza*	*(x)*	*thubutu*

E. Kupigia mstari jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika maswali ya kujaza nafasi wazi ubaoni. Washirikishe wanafunzi kujaza majibu kwa kupigia mstari jibu sahihi.

(ii) Waongoze wanafunzi kujadili na washirikishe kurekebisha makosa yanayojitokeza.

(iii) Toa maelezo ya mifano ukurasa wa **114** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **114** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 110 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) kwa (ii) ndani ya (iii) wangu (iv) alikula (v) atamtumia
(vi) aliitisha (vii) ndiye (viii) shule (ix) kamwe (x) anakwenda

F. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kuunda neno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika maneno yaliyochanganywa herufi ubaoni.

(ii) Waongoze wanafunzi kupanga herufi ili kupata neno au maneno sahihi.

(iii) Wape nafasi wanafunzi wajaribu kadiri inavyowezekana.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **115** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*chutama*	*(vi)*	*kithiri*
(ii)	*miminika*	*(vii)*	*jihimu*
(iii)	*fani*	*(viii)*	*amini/imani*
(iv)	*thubutu*	*(ix)*	*ngome*
(v)	*kamwe / mwake*	*(x)*	*ng'ambo*

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi mambo ya kuzingatia katika kufanya ufupisho.

(b) Waongoze wanafunzi kurudia kusoma hadithi ya **Maisha ya kuku.**

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A na 5 B lililopo ukurasa wa **115** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu zoezi la 5 A:

(i) (iv) (ii) (v) (iii) (i) (iv) (iii) (v) (ii)

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 111 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Nne

Kumbukumbu za mikutano

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza namna ya kuandika kumbukumbu za mikutano. Pia, atajifunza elimu ya afya na uzazi na kufanya mazoezi mbalimbali ya lugha.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma hadithi ya **Kisiwa cha Masaibu**
(b) kubaini muundo wa kumbukumbu za mkutano
(c) kueleza umuhimu wa kumbukumbu za mkutano
(d) kuandika kumbukumbu za mkutano
(e) kutunga insha ya elimu ya afya na uzazi

Mahitaji: vitu halisi, picha, vitendo, bangokitita, nakala za kumbukumbu za mikutano na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri*, ukurasa wa **116** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Lengo ni kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza na kufahamu uelewa walio nao wanafunzi kuhusu somo utakalolifundisha.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya hadithi ya **Kisiwa cha Masaibu** iliyopo ukurasa wa **116 - 122** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi wasimulie kwa maneno machache habari waliyoisoma.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 112 26/07/2021 12:02

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi kanuni na taratibu za kusoma kwa sauti kwa kuzingatia alama za uandishi.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu, bila kujali jinsi na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo: *dhoruba, nahodha, furukuta, kimuyemuye, maradhi, gugumia, fakamia, mandhari, fukwe* na *balehe.*

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome.

(c) Onesha picha ya mambo mbalimbali yahusuyo umuhimu wa elimu, afya bora, uzazi na maradhi.

(d) Wape wanafunzi muda wa kuzichunguza.

(e) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya neno mojamoja.

(f) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo. Wanafunzi watunge sentensi kwa kuzungumza. Andika sentensi hizo ubaoni.

(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **122** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao. Sentensi ziwe tofauti na zile zilizotolewa mifano.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 113 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na maana zake.

(b) Nakili ubaoni zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **123** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma nahau zote.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **123** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(e) Waongoze wanafunzi katika makundi, kutafuta nahau nyingine tano na kueleza maana zake.

Majibu:

1. *simama*
2. *enda upandeupande*
3. *amua / toa uamuzi*
4. *fanya mtu awe na hamu ya kufanya jambo*
5. *vumilia*

Somo la 5: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.

(b) Waongoze wanafunzi kujibu swali la kwanza hadi la nne kwenye zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **123** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wanafunzi wajibu maswali hayo kwa kuzungumza.

(c) Waongoze wanafunzi kumalizia maswali yaliyobaki kwenye zoezi hili kwenye madaftari yao.

Majibu:

1. *kuwashusha. [MHINDI]*
2. *hatarini. [KINYONGA]*
3. *hushauriwi. [KIFO] / [KUZALIWA]*
4. *faida. [NYWELE] / [NYOTA] / [MCHANGA]*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 114 26/07/2021 12:02

5. *wanaingia. [MZINGA NA NYUKI]*
6. *haridhiki. [TUMBO]*
7. *sinema. [NDOTO]*
8. *linapokuchwa / linapozama. [NYUMBA]*
9. *haupandiki. [MOSHI]*
10. *hawana. [VYURA]*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kujaza herufi zinazoendana na namba ili kupata maneno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma herufi na namba kama zinavyoonekana kwenye jedwali.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi hili, ukurasa wa **123 - 124** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*MKUTANO*	*(vi)*	*WEWE*
(ii)	*RAMANI*	*(vii)*	*KIELEZI*
(iii)	*KATIBU*	*(viii)*	*KIJANA*
(iv)	*NOMINO*	*(ix)*	*ZAWADI*
(v)	*TUNGO*	*(x)*	*ELIMU*

B. Kubadili sentensi ziwe katika wakati uliopo na wakati uliopita

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi hizo kwa usahihi kwenye vitabu vyao.

(ii) Waulize ili wataje wakati wa kila sentensi wanayoisoma.

(iii) Wanafunzi wanaposoma na kutaja aina ya wakati uliotumiwa katika sentensi, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo. Kumbuka kuwa silabi zinazoonesha nyakati katika kitenzi ni 'na' (wakati uliopo), 'li' (wakati uliopita) na 'ta' (wakati ujao).

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 115 26/07/2021 12:02

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 5 B, ukurasa wa **124 - 125** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

C. Kuandika neno lingine linalofanana na maneno uliyopewa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kusoma maneno kwa usahihi kwenye vitabu vyao.

(ii) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi hilo, ukurasa wa **125** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) tumbukiza / penyeza / pitisha
(ii) shangwe / shamrashamra / hoihoi / kayaya / ramsa / mteremo / zumo
(iii) kera / ghasi / taabisha / hangaisha / bughudhi / tesa / dhili / goga / kefya
(iv) chomoza / zuka / tokea
(v) msitu
(vi) sigina / pondaponda
(vii) chanzo / chimbuko / kitovu / msingi / sababu / usuli / chipuko
(viii) aibu / twezo / kashfa / tahayuri / izara / nazaa / hizaya / junaa
(ix) seti / cheuzi
(x) dhiki / matatizo / adhabu / balaa / janga / taabu / masumbuko / usumbufu / udhia / mushkili / mzingile

D. Kutaja aina ya neno mojamoja lililotumiwa katika sentensi. Kuandika chini ya neno hilo herufi inayowakilisha aina ya neno hilo

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kutaja aina za maneno na vifupi vyake, kisha viandike ubaoni. Wakati wanafunzi wanataja aina za maneno na vifupi vyake, baini makosa na yasahihishe papo hapo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 116 26/07/2021 12:02

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti sentensi hizo kumi.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **125** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Mvua ilinyesha siku nzima.*
N T E

(ii) *Viwavijeshi wamemaliza mahindi yetu.*
N T N V

(iii) *Wanafunzi wangu wamechaguliwa wote.*
N V T E

(iv) *Vitunguu saumu vinanukia vizuri.*
N V T E

(v) *Mlango wa darasa umejibamiza.*
N H N T

(vi) *Tutaenda mtoni kuchota maji.*
T E T N

(vii) *Umeme hutuletea maendeleo.*
N T N

(viii) *Mwakani tutafanya mtihani wa Darasa la Saba.*
E T N H N H N

(ix) *Mwindaji alimlenga vizuri mnyama.*
N T E N

(x) *Aa! Unanisingizia.*
Hs T

(xi) *Yeye ni nani?*
W t W

E. Kutumia silabi “ri” au “li” kukamilisha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika herufi r na l ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kuzitamka kwa usahihi.

(ii) Wanafunzi wanapotamka herufi r na l, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo. Kumbuka kuwa konsonanti hizo hutamkiwa kwenye ufizi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 117 26/07/2021 12:02

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *ripoti*
(ii) *mawasiliano*
(iii) *asali*
(iv) *risala*
(v) *linda / rinda (rinda = mkunjo wa nguo au kanzu ya kike)*
(vi) *limau*
(vii) *lori*
(viii) *malaria*
(ix) *reli*
(x) *siri / sili (sili = kutotia chakula kinywani na kutokimeza)*
(xi) *serikali*
(xii) *ramli*

F. Kuondoa silabi moja katika maneno ili kupata maneno mapya yaliyo sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi watunge maneno mapya kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 5 F, ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F kwenye madaftari yao lililopo ukurasa wa **126** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *tasa/ kisa / kita*
(ii) *ua*
(iii) *dua*
(iv) *sifu / sia / afu*
(v) *zama / tama*
(vi) *mfu / kufu*
(vii) *uza / uzi*
(viii) *swali / mali*
(ix) *yote*
(x) *hapoi*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 118 26/07/2021 12:02

G. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano kwa kuandika sentensi ubaoni ili wanafunzi wachague jibu lililo sahihi.

Mfano:

(i) *Mtu anayeandika kumbukumbu za mikutano huitwa katibu.*
   (a) *Katibu*
   (b) *Mwenyekiti*
   (c) *Mtunzi*
   (d) *Kumbukizi*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **126 - 127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu: *(i) katibu (ii) muhtasari (iii) 3 (iv) kutunza taarifa za mambo muhimu yaliyojadiliwa katika mkutano (v) insha*

Kumbuka mwanafunzi anaweza kuandika herufi za majibu sahihi pia.

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 6 A na 6 B lililopo ukurasa wa **127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Tumia maswali na vipengele vilivyoorodheshwa kwenye swali la 6 A na 6 B kuongoza mjadala.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A na 6 B lililopo ukurasa wa **127** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo, muundo wa kumbukumbu za mkutano, muundo wa insha, na matumizi ya herufi kubwa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 119 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Tano

Umiliki katika lugha

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atasoma habari inayohusu **kijiji chao**. Pia, atajifunza maneno yanayoonesha umiliki. Vilevile, atajifunza kuyatumia maneno hayo katika sentensi na kifungu cha habari. Aidha, atajifunza msamiati, nahau, mazoezi mbalimbali ya lugha na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari inayohusu **kijiji chao**
(b) kutumia maneno yanayoonesha umiliki katika sentensi na kifungu cha habari
(c) kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yanayoonesha umiliki

Mahitaji: vitu halisi, kadi za maneno yanayoonesha umiliki, kalamu rashasha, bangokitita na picha (za kawaida na za mguso)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo kwenye kipengele cha *fikiri* ukurasa **128** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Kijiji chao** iliyopo ukurasa wa **128 - 131** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Wanakijiji walikuwa na maendeleo gani?
    (ii) Dungo alimwambia nini rafiki yake?
    (iii) Wanakijiji walijitoleaje katika ujenzi wa wodi ya watoto na akina mama wajawazito?
(d) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 120 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **131** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi, na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudirudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika maneno yafuatayo ubaoni: *miliki, hamasisha, stawi, mchango*, *zahanati, kero, mganga, wodi, kliniki* na *paa*. Waongoze wanafunzi kuyasoma na kueleza maana ya neno mojamoja.

(b) Fundisha maneno hayo kwa kutumia mbinu ya maelezo, kadi za maneno, vitu halisi, picha na maigizo.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **131** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa katika mfano.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 121 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Imla

Hatua za ufundishaji

(a) Wakumbushe wanafunzi matumizi sahihi ya alama za uandishi, mwandiko mzuri, mpangilio wa aya na nafasi kati ya neno na neno.

(b) Soma kwa sauti kifungu cha maneno kwa kuzingatia alama za uandishi huku wanafunzi wakisikiliza.

> *Nipuro ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mkomaindo iliyopo Wilaya ya Masasi, Mtwara. Baba yake ni askari. Mama yake ni nesi. Siku ya Jumamosi, humsaidia dada yake anayeitwa Irusho kufanya kazi mbalimbali za nyumbani. Baada ya kumaliza kazi zake, huenda kuwatembelea rafiki zake. Rafiki zake Nipuro ni Nehata, Pichikina, Nikosho na Nihawo. Wakati wa likizo, Nipuro huenda kumtembelea bibi yake ambaye anaitwa Nipampa. Nipampa anaishi Kijiji cha Makosho. Yeye ni mkulima wa korosho, mbaazi, mihogo na choroko. Nipuro anapenda sana kula korosho. Siku moja alimuuliza bibi yake, "Bibi, kwa nini unalima korosho?" Bibi yake alimjibu, "Mjukuu wangu, ninalima korosho ili kujiongezea kipato."*

(c) Soma tena hatua kwa hatua huku wanafunzi wakiandika.

(d) Soma kifungu chote kwa mara ya tatu ili wanafunzi wafanye masahihisho kabla kazi zao hazijasahihishwa.

(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa maneno, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, alama za uandishi, hati ya wima ya kuunga, matumizi ya herufi kubwa na usafi wa kazi.

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya nahau kwa kutumia mifano iliyopo zoezi la 3 ukurasa wa **131 - 132** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja nahau mbalimbali na kueleza maana zake na kutunga sentensi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **131 - 132** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 122 26/07/2021 12:02

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi. Tumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **132** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **132** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*chake*	(v)	*yao*	(ix)	*yao*	(xiii)	*yao*
(ii)	*zetu*	(vi)	*lake*	(x)	*letu*	(xiv)	*wangu*
(iii)	*lake*	(vii)	*yetu*	(xi)	*wetu*	(xv)	*yake*
(iv)	*yake*	(viii)	*vyake*	(xii)	*zangu*		

B. Kuandika umoja au wingi wa maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **133** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza wanafunzi dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **133** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i)	*karatasi*	*(vi)*	*galoni*
(ii)	*ungo*	*(vii)*	*likizo*
(iii)	*shamba*	*(viii)*	*changu*
(iv)	*mpini*	*(ix)*	*ndizi*
(v)	*vikapu*	*(x)*	*mboga*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 123 26/07/2021 12:02

C. Kubadili sentensi kuwa katika hali ya mazoea

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu hali ya mazoea.

(ii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi ziwe katika hali ya mazoea.

(iii) Tumia mifano iliyopo ukurasa wa **133** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **133** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Babu Mpande hupanda maua nyumbani kwake.*
(ii) *Gari la mjomba hutoa moshi mwingi.*
(iii) *Wakulima hupalilia mikorosho mara mbili kwa mwaka.*
(iv) *Mbwa wetu hubweka akiona wageni.*
(v) *Dada yangu hufanya mazoezi kila siku asubuhi.*
(vi) *Shangazi huja na mtoto wake nyumbani.*
(vii) *Mtoto wa mjomba huitwa binamu.*
(viii) *Joni hutembelea daraja la Mto Rufiji wakati wa likizo.*
(ix) *Mvua nyingi hunyesha msimu wa masika.*
(x) *Kaka hujibu barua zote alizoandikiwa na rafiki zake.*

D. Kupigia mstari kivumishi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo zoezi la 4 D swali la (i - xii) ukurasa wa **133 - 134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kupigia mstari vivumishi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye zoezi la 4 D.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **133 - 134** Katika kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Mwanafunzi <u>hodari</u> anajua kusoma vizuri.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 124 26/07/2021 12:02

(ii) Uchafu wote umemwagwa mbali.
(iii) Mpira wetu umepotea kabisa.
(iv) Mboga zote za majani ni nzuri.
(v) Mama yao ni mpole.
(vi) Shule ile ina walimu wengi.
(vii) Wimbo huu ni mzuri.
(viii) Kiranja huyu amepata kura nyingi.
(ix) Nyumba hii inapangishwa.
(x) Watu hawa wana ushirikiano kama siafu.
(xi) Babu Mapande ana mashamba makubwa ya mpunga.
(xii) Mjukuu wangu anapenda kulia.

E. Kutunga sentensi sahihi kumi (10) kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelekezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Chora ubaoni jedwali lililopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma maneno ya safu ya kwanza, ya pili na ya tatu.
(iv) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi sahihi kwa kutumia jedwali hilo.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

F. Kuandika maneno matano yenye maana kutokana na jedwali na kutunga sentensi moja kwa kila neno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Chora ubaoni jedwali lililopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Zungushia herufi Z, O, na A kama inavyoonekana kwenye jedwali ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iv) Waongoze wanafunzi kusoma neno lililopatikana kutokana na herufi hizo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 125 26/07/2021 12:02

(v) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia neno zoa.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

G. Kupanga herufi zilizochanganywa ili kupata neno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Andika ubaoni herufi zilizopo kwenye kila neno katika zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **134 - 135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kusoma herufi hizo zinazounda kila neno.
(iv) Waongoze wanafunzi kupanga herufi kwa kutumia mifano iliyopo ukurasa wa **134** katika Kitabu cha Mwanafunzi ili kupata neno sahihi. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **134 - 135** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i)	*soma*	*(vi)*	*miche*
(ii)	*bidii*	*(vii)*	*panga*
(iii)	*osha*	*(viii)*	*sepetu*
(iv)	*magogo*	*(ix)*	*nishati*
(v)	*azima*	*(x)*	*safari*

H. Kupanga sentensi katika mtiririko wenye kuleta maana

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zilizopo zoezi la 4 H ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Waongoze wanafunzi kupanga sentensi katika mtiririko wenye kuleta maana kwa mazungumzo.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 H lililopo ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Jumamosi iliyopita mama alinituma sokoni.*
(ii) *Aliniambia ninunue nyanya, vitunguu, sukari, mchele na mafuta.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 126 26/07/2021 12:02

(iii) *Nilipokuwa njiani, nilimwona nyoka.*
(iv) *Niliogopa, lakini nilipiga moyo konde.*
(v) *Nilirudi nyuma kidogo nikaokota fimbo.*
(vi) *Nilimpiga nyoka kwa ile fimbo akafa.*
(vii) *Nilikimbia hadi sokoni.*
(viii) *Nilipokuwa ninarudi, niliwakuta kunguru wanamla yule nyoka niliyemuua.*
(ix) *Nilikimbia hadi nyumbani.*

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(b) Ongoza majadiliano kuhusu maneno yanayoonesha umiliki na namna yanavyoweza kutumika katika kuandika utungaji.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kilichopo kwenye zoezi la 5 ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kuweka majibu.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **135** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi na mtiririko wa mawazo.

Majibu:

Wavuvi walichukua nyavu zao kuelekea ziwani. Walipofika huko, walikuta wavuvi wengine wameshaingia kwenye mitumbwi yao. Kando ya ziwa, kulikuwa na wachuuzi mbalimbali wakiwa na vikapu vyao mikononi. Wachuuzi hao walikuwa wanawasubiri kwa hamu wavuvi watoke ziwani. Baada ya muda, wavuvi waliwasili na mitumbwi yao ikiwa imejaa samaki wa kila aina. Walipofika ufukweni, walianza kuuza samaki wao kwa wachuuzi. Kila mvuvi alipanga bei yake kulingana na ukubwa wa samaki. Wachuuzi walinunua samaki kulingana na vipato vyao. Baada ya shughuli ya kununua na kuuza samaki, kila mmoja alishika njia yake. Wachuuzi wengine walikwenda kuuza samaki wao wakiwa wabichi, wengine walikwenda kuwauza baada ya kuwakaanga.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 127 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Sita

Kuandika habari

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu kazi mbalimbali zinazofanyika katika jamii yake. Pia, atasoma habari kuhusu **likizo yangu** na kufanya mazoezi mbalimbali.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kutaja kazi mbalimbali zinazofanyika katika jamii yake
(b) kusoma habari na kujibu maswali
(c) kutunga habari fupi kuhusu kazi mbalimbali zinazofanyika katika jamii yake

Mahitaji: vitu halisi, kadi za maneno, kalamu rashasha, bangokitita na picha (za kawaida na za mguso)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **136** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Lengo la maswali ya fikiri ni kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza pamoja na kupata uelewa wa mwanzo alionao mwanafunzi kuhusu somo utakalolifundisha.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Likizo yangu** iliyopo ukurasa wa **136 - 138** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Habari uliyoisoma, inahusu nini?
    (ii) Nyakitwe anasoma shule gani?
    (iii)Dada yake Nyakitwe anafanya kazi gani?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 128 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **137** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Swali lifuatalo litakuongoza: Unaona nini katika picha hiyo?
(f) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **139** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *shirika, gutuka, barizi, uhandisi, damka, nanga, bobea*, *daladala na kivuko* kwa kutumia vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.
(b) Waongoze wanafunzi kuoanisha msamiati na maana zake kwenye zoezi la pili lililoko ukurasa wa **139** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kusoma msamiati na kueleza maana zake kwa kuzungumza.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 129 26/07/2021 12:02

(d) Angalia usahihi wa msamiati na maana zake.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **139** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha misamiati na maana zake ni sahihi.

Majibu:

(i)	*c*	(iv)	*d*	(vii)	*f*
(ii)	*j*	(v)	*i*	(viii)	*b*
(iii)	*h*	(vi)	*e*	(ix)	*g*

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kuchagua jibu sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano kwa kuandika swali ubaoni ili wanafunzi wachague jibu lililo sahihi.

Mfano: *Mtu anayeendesha meli huitwa <u>nahodha</u>.*

(a) *rubani*
(b) *nahodha*
(c) *dereva*
(d) *mhadhiri*

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A lililopo ukurasa wa **140 - 141** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*a*	(vi)	*b*
(ii)	*b*	(vii)	*a*
(iii)	*d*	(viii)	*a*
(iv)	*c*	(ix)	*d*
(v)	*d*	(x)	*d*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 130 26/07/2021 12:02

B. Kutumia maneno yaliyoko kwenye kisanduku kukamilisha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Chora kisanduku ubaoni au kwenye bangokitita na uandike maneno yatakayotumika kukamilisha sentensi kwenye kisanduku hicho.

(ii) Andika ubaoni au kwenye bangokitita mfano uliopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia mfano uliopo ubaoni au kwenye bangokitita.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **141 - 142** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*mkalimani*	(vi)	*seremala*	(xi)	*dobi*
(ii)	*sonara*	(vii)	*mkunga*	(xii)	*machinga*
(iii)	*hakimu*	(viii)	*mfinyazi*	(xiii)	*mwindaji*
(iv)	*mwashi*	(ix)	*daktari*	(xiv)	*mvuvi*
(v)	*mfugaji*	(x)	*kocha*		

C. Kuandika visawe vya maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu maneno yenye maana sawa.

(ii) Andika ubaoni neno la mfano kutoka katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kisawe chake.

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja kisawe cha neno hilo.

(iv) Andika ubaoni kisawe cha neno hilo.

(v) Waongoze wanafunzi kusoma kwa sauti neno na kisawe chake.

(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **142** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*maafikiano, mkataba*	(vi)	*milele*
(ii)	*ukwasi*	(vii)	*changanyika*
(iii)	*asili,chimbuko*	(viii)	*upesiupesi, harakaharaka*
(iv)	*fitina*	(ix)	*haba*
(v)	*shuka*	(x)	*dosari, doa*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 131 26/07/2021 12:02

D. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila kinyume chake.

Mfano: *(a) safisha……..*

(b) ukweli ……

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iii) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.

(iv) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **142 - 143** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i) muuzaji

(ii) tawanya / sambaza / tapanya

(iii) fupisha

(iv) fumbua

(v) haribu

(vi) kashifu

(vii) pangua

(viii) funua

(ix) chuki

(x) ugua

E. Kujaza chemshabongo kwa kuzingatia maelezo ya kwenda chini na kulia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya somo litakalofundishwa.

(ii) Nakili chemshabongo na maelekezo ya kwenda chini na kulia ubaoni au kwenye bangokitita kama yalivyo katika zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **143 - 144** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Toa mfano wa kwenda kulia wa swali la kwanza kwa kuuliza swali lifuatalo:

1. Mtu anayetunga na kuimba mashairi (herufi 7) - MSHAIRI

(iv) Andika jibu hilo kwenye vyumba vya kuanzia namba 1 kwenda kulia. Kila chumba kiandikwe herufi moja tu. Tumia herufi kubwa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **143 - 144** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 132 26/07/2021 12:02

Majibu:

[1]M	[2]S	[3]H	A	I	[4]R	I		[5]I	
[6]S	I	A			E			N	
[7]U	M	W	A		[8]F	A	N	I	
S	U	A		[9]A	A				
I				G			[10] D		[11]M
				A			O		K
[12]R	U	B	A	N	I		B		A
				O			I		L
									I
[13]M	H	A	S	I	B	[14]U			M
						[15]Z	I	B	A
[16]M	V	U	V	I		I			N
							[17]B	E	I
[18]M	K	U	T	U	B	I			
							[19]P	O	A
[20]M	B	U	N	G	E				

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja kazi wanazozipenda na kueleza sababu za kupenda kazi hizo.

(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia katika uandishi wa habari.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **144** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa kuzingatia mtiririko na idadi ya maneno.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo yanayoendana na kazi husika na matumizi sahihi ya herufi kubwa. Pia, zingatia idadi ya maneno.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 133 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Saba

Shairi la mabadiliko ya hali ya hewa

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa. Atajifunza kutunga na kughani shairi pamoja na kusimulia kisa kinachohusu mabadiliko ya hali ya hewa.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari kuhusu **mabadiliko ya hali ya hewa** na kujibu maswali ya ufahamu
(b) kutunga mashairi ya kimapokeo kuhusu hali ya hewa
(c) kughani mashairi ya kimapokeo yaliyotungwa
(d) kusimulia kisa kinachohusu mabadiliko ya hali ya hewa

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya msamiati, kalamu na daftari

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **145** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari inayohusu **mabadiliko ya hali ya hewa** iliyopo ukurasa wa **145 - 148** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Ongezeko la joto husababishwa na nini?
    (ii) Matera anapenda kuchunga nini?
(d) Waongoze wanafunzi wajadili picha iliyopo ukurasa wa **146** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 134 26/07/2021 12:02

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza ukurasa wa **148** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Wakumbushe wanafunzi wazingatie alama za uandishi na matamshi fasaha ya Kiswahili wanaposoma kwa sauti.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha papo hapo.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri inavyowezekana.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika maneno yafuatayo ubaoni: *ngurumo, rindima, dhoruba, pazia, ukame, njaa, fukaa, hakahaka, shaua, gharika, gubika* na *tajirika,* kisha wanafunzi wayasome na kueleza maana ya neno mojamoja.
(b) Fundisha maneno hayo kwa kutumia vitu halisi, maelezo, picha na maigizo.
(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.
(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 135 26/07/2021 12:02

wa **149** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga, hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mifano.

Somo la 4: Mazoezi ya lugha

A. Kukanusha sentensi, kisha kupigia mstari neno lililokanushwa

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 3 A ukurasa wa **149** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 A ukurasa wa **149** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Matera <u>hampendi</u> babu yake.

(ii) Babu <u>hapendi</u> kuimba shairi.

(iii) <u>Hawakula</u> chakula kitamu.

(iv) <u>Hatupaswi</u> kuwapenda na kuwajali maadui.

(v) Matera <u>hasomi</u> Darasa la Sita.

(vi) Mvua <u>haikunyesha</u> kwa kishindo.

(vii) Radi <u>si</u> rafiki kwa maisha ya binadamu.

(viii) Doto <u>hakung'atwa</u> na nyuki jana akiwa shambani.

(ix) Nyumba <u>haikuezuliwa</u> na upepo.

(x) Mimi <u>sikufurahia</u> safari ya kwenda kwa babu.

B. Kuandika wingi wa sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu umoja na wingi.

(ii) Tumia swali la kwanza kama mfano katika zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa **149** katika Kitabu cha Mwanafunzi kuwaelekeza dhana ya umoja na wingi. Unaweza kuongeza mifano mingine.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 B lililopo ukurasa wa

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 136 26/07/2021 12:02

149 - 150 katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(iv) Sahihisha madaftari yao huku ukirekebisha dosari unazozibaini kwa kila mwanafunzi.

Majibu:

(i) Sisi ni watoto wadogo.
(ii) Wanafunzi wanapaswa kuwa na heshima.
(iii) Mashairi yanavutia.
(iv) Chui ni wanyama hatari.
(v) Ukungu ulitugubika; hatukuweza kuona mbele.
(vi) Watoto wanajua kuruka.
(vii) Walimu wanasoma magazeti.
(viii) Wazee wanaimba nyimbo vizuri.
(ix) Wale wanajua kusoma vizuri.
(x) Vyakula viliungwa kwa nyanya zilizoiva.

C. Kuandika NDIYO au HAPANA katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano ya maswali yenye majibu ya NDIYO au HAPANA.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 C lililopo ukurasa wa **150** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*NDIYO*	*(v)*	*HAPANA*	*(viii)*	*NDIYO*
(ii)	*NDIYO*	*(vi)*	*NDIYO*	*(ix)*	*NDIYO*
(iii)	*HAPANA*	*(vii)*	*HAPANA*	*(x)*	*NDIYO*
(iv)	*HAPANA*				

D. Kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jumla kuhusu namna ya kubadili sentensi kuwa katika kauli taarifa. Waambie wanafunzi kuwa kauli taarifa ni maneno yanayozungumzwa na msemaji wa pili ambaye ni mtoa taarifa. Mtoa taarifa hutumia neno *kuwa* au *kwamba* ili kutoa taarifa.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 137 26/07/2021 12:02

Mfano: Kauli halisi: *Baba alisema, "Nitakununulia kabati la kutunzia vyombo."*

Kauli taarifa: *Baba alisema kuwa ataninunulia kabati la kutunzia vyombo.*

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 3 D ukurasa wa **150** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 D lililopo ukurasa wa **150 - 151** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Mjomba amesema kwamba mwaka huu atavuna mazao mengi.

(ii) Amina aliniambia kwamba kaka yangu ni mkorofi sana.

(iii) Kinyonga alitueleza kwamba hatahudhuria mkutano.

(iv) Dada aliniambia kwamba atanileta zawadi.

(v) Bibi alisema kuwa njugu mawe zote zimeisha shambani.

(vi) Mtoto alisema kuwa kesho watakula ubwabwa kwa maharage.

(vii) Mtoto alituarifu kuwa mti umeanguka mtoni.

(viii) Mwanafunzi alisema kuwa yeye atachezea timu ya Taifa.

(ix) Babu alisema kuwa mwaka huu kilimo kimekubali sana.

(x) Mwalimu alitueleza kuwa Kiswahili kinafundishwa hadi nje ya nchi yetu.

E. Kuzungushia herufi katika jedwali kupata maneno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo katika zoezi la 3 E ukurasa wa **151** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Toa maelezo ya namna ya kuunda maneno sahihi kutokana na jedwali hilo.

(iii) Toa mfano kwa kuzungushia herufi zinazounda neno la Kiswahili.

(iv) Waongoze wanafunzi kuzungushia herufi zote zinazounda

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 138 26/07/2021 12:02

maneno yote sahihi ya Kiswahili yaliyomo kwenye jedwali.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 E lililopo ukurasa wa **151** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

(vi) Buni jedwali linaloshabihiana na lile lililopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi ili kuunda maneno mengine ya Kiswahili.

Majibu:

D	H	U	L	U	M	A	H
H	U	R	I	A	H	M	CH
A	S	O	N	L	A	A	A
H	I	G	R	I	S	N	I
A	S	O	I	M	I	I	R
M	H	P	M	U	B	E	L
A	A	A	U	U	U	A	E

Mwanafunzi anaweza kuzungushia herufi nyingine ili kuunda maneno mengine pia.

F. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyoko kwenye kisanduku

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia swali la kwanza kama mfano lililopo kwenye zoezi la 3 F ukurasa wa **151** katika Kitabu cha Mwanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

(ii) Waongoze kufanya zoezi la 3 F lililopo ukurasa wa **151 - 152** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) ngurumo
(ii) mbuzi
(iii) upinde wa mvua
(iv) kimbunga
(v) chui
(vi) pango
(vii) radi
(viii) ukame
(ix) ghani
(x) msanii

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 139 26/07/2021 12:02

G. Kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu kutoka kwenye mabano

Hatua za ufundishaji

(i) Waelekeze wanafunzi kwa mifano jinsi ya kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano na kujaza katika nafasi zilizoachwa wazi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 G lililopo ukurasa wa **152 - 153** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*perege*	*(v)*	*kitabu*	*(viii)*	*hucheza*
(ii)	*kizuri*	*(vi)*	*hutaga*	*(ix)*	*tulishangilia*
(iii)	*kaka*	*(vii)*	*ndiye*	*(x)*	*ameukata*
(iv)	*kinyonga*				

H. Kuandika kinyume cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni maneno machache bila vinyume vyake.

Mfano: *cheka - nuna*

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja vinyume vya maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iii) Andika ubaoni majibu yaliyotajwa na wanafunzi.

(iv) Angalia usahihi wa majibu hayo.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 H lililopo ukurasa wa **153** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Majibu:

(i)	*kimya*	*(v)*	*punguza*	*(viii)*	*bandua*
(ii)	*kunjua*	*(vi)*	*nuru, mwanga*	*(ix)*	*funua*
(iii)	*anua*	*(vii)*	*pangua*	*(x)*	*fumbua*
(iv)	*vua*				

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 140 26/07/2021 12:02

Somo la 5: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Andaa shairi lenye beti tano linalohusu *mabadiliko ya hali ya hewa,* kisha ulitumie kama mfano wa kutunga shairi.

(b) Shairi lisomwe na lighanwe.

(c) Waongoze wanafunzi kusoma na kughani mstari kwa mstari. Kila mstari una idadi ya silabi 16. Silabi hizi huitwa *mizani.* Waongoze wanafunzi kuhesabu mizani hizo.

(d) Waelekeze wanafunzi kuwa, katika ubeti mwishoni mwa kila mstari, zipo sauti zinazofanana au zinazolingana kwa jinsi zinavyotamkwa na kuandikwa. Silabi hizi huitwa *vina.* Wanapoghani, wazitamke kwa mkazo ili kuleta muwala wa shairi.

(e) Waongoze wanafunzi kutaja vina katika kila ubeti.

(f) Waelekeze wanafunzi kuwa mstari wa mwisho katika ubeti huitwa *kituo*.

(g) Waongoze wanafunzi kuzungumzia zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **153** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wanafunzi wataje maneno na mafungu yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa.

(h) Andika ubaoni kila neno au fungu linalotolewa na wanafunzi kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa.

(i) Waongoze wanafunzi kupanga maneno yote kwa utaratibu wa ulingano wa silabi za mwisho wa maneno, yaani utaratibu wa urari au ulinganifu wa vina.

(j) Waongoze wanafunzi kutunga ubeti mmoja wa mfano kwa kutumia maneno hayo na mengine.

(k) Waelekeze wanafunzi kutunga beti tatu za shairi la kimapokeo kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutumia ubeti mmoja wa mfano.

(l) Waongoze wanafunzi kughani shairi hilo la kimapokeo la beti tatu walizotunga.

(m) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A na B lililopo ukurasa wa **153** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(n) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia kanuni za utungaji wa shairi la kimapokeo. Rekebisha kila dosari unayoibaini. Chagua beti mbili au tatu ambazo zimetungwa na kuandikwa vizuri ili zisomwe na kughanwa darasani.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 141 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Nane

Kusikiliza habari ya madhara ya rushwa

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atasisitizwa zaidi stadi ya kusikiliza. Pia, atajifunza kuhusu madhara ya rushwa na namna ya kupambana nayo. Vilevile, atafanya mazoezi mbalimbali ya lugha na kutunga habari kuhusu rushwa.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma na kusikiliza habari inayohusu **Pete ya Mtemi Ndamanga**
(b) kumalizia methali
(c) kutunga sentensi kwa kutumia nahau
(d) kufanya mazoezi mbalimbali ya lugha
(e) kutunga habari kuhusu rushwa

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), bangokitita na kalamu rashasha

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo kwenye kipengele cha *fikiri* ukurasa **154** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari inayohusu Pete ya Mtemi Ndamanga iliyopo ukurasa wa **154 - 157** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole wala kutoa sauti.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Pete iliyopotea ilikuwa ya nani?
    (ii) Unafikiri ni mazingira gani yanaweza kusababisha rushwa?
(d) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 142 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **157 - 158** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza ni kitu gani unatarajia kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu alama za uandishi kwa kuuliza maswali.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na kuzirekebisha.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda kisha rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha misamiati ifuatayo*: ng'amua, mnyamapori, karamu, hongo, charazwa, henzirani* na *msumeno* kwa kutumia maelezo, kadi za maneno, vitu halisi, picha na maigizo.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, kisha wanafunzi wayasome na waongoze kueleza maana ya neno mojamoja.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa kuzungumza kwa kutumia maneno hayo, kisha andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Kagua usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

Mfano: *Juma alikata mti mkubwa kwa kutumia msumeno.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 143 26/07/2021 12:02

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **158** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga, hazifanani na zile zilizotolewa mfano.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia swali la kwanza la zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **158** katika Kitabu cha Mwanafunzi kama mfano.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo katika ukurasa wa **158 - 160** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*a*	*(iv)*	*b*	*(vii)*	*b*	*(ix)*	*b*
(ii)	*c*	*(v)*	*c*	*(viii)*	*d*	*(x)*	*b*
(iii)	*d*	*(vi)*	*a*				

Somo la 5: Nahau

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja nahau wanazozifahamu na kutoa maana zake.

(b) Nakili ubaoni nahau zilizopo ukurasa wa **160** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(c) Tumia mifano iliyopo katika zoezi hilo ili kuonesha jinsi ya kutunga sentensi kwa kutumia nahau.

(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **160** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kujaza maneno kwenye chemshabongo kulingana na maelekezo

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **160 - 161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 144 26/07/2021 12:02

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maelekezo ya kwenda chini na kulia.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **160 - 161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

Kwenda chini

1. NYATI
3. TETEMA

Kwenda kulia

2. PETE
4. TEMBEA
5. MAYAI

B. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kukanusha sentensi kwa kutumia mifano iliyopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi. Kumbuka hali timilifu na wakati uliopo kwenye ukanushi utatumia silabi "ja" kwenye kitenzi. Wakati uliopita utatumia silabi "ku" kwenye kitenzi.
(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

C. Kupigia mstari vielezi vilivyopo katika kifungu cha habari

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.
(ii) Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari kilichopo ukurasa wa **161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(iii) Toa mifano ya vielezi na uviandike ubaoni.
(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 145 26/07/2021 12:02

Majibu:

Juma na Roda ni watoto wazuri. Bibi yao huwahimiza kwenda shuleni. Juma na Roda wana bidii sana katika masomo. Wao hufanya vizuri kwenye masomo yao. Shuleni, wanapendwa na walimu pamoja na marafiki zao. Juma na Roda wanawatii walimu wao. Pia, wanamtii bibi yao. Bibi akiwaagiza waende kuteka maji, wote kwa pamoja huenda kuteka maji. Wakishaleta maji nyumbani, bibi huwapongeza. Mara kwa mara, bibi huwasimulia hadithi jioni.

D. Kubadili kauli taarifa kuwa kauli halisi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo ya jumla kuhusu namna ya kubadili kauli taarifa kuwa kauli halisi.

(ii) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 5 D uliopo ukurasa wa **161** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kujua kuwa kauli halisi inatoka kwa msemaji wa kwanza na kauli taarifa ni ya mtu anayetoa taarifa kuhusu maneno ya msemaji wa kwanza.

Mfano: Kauli taarifa: *Baba alisema kwamba atanisomesha.*

Kauli halisi: *Baba alisema, "Nitakusomesha."*

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **161 - 162** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Mama aliguna na kusema, "Usiende tena kuzurura barabarani."*

(ii) *Alisema, "Nipeni chakula changu."*

(iii) *Aliwaambia, "Mwenyekiti atahutubia mkutano."*

(iv) *Furaha alisema, "Bora niache kazi."*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 146 26/07/2021 12:02

(v) *Mzee Mwaka alimwambia Adili, "Rushwa ni adui wa haki."*

(vi) *"Kila kazi ina changamoto zake." Amina alisisitiza.*

(vii) *Mzee Mwande alisema, "Ni lazima nimsomeshe binti yangu ili aelimike."*

(viii) *"Naomba mjenge wodi mbili." Daktari alituomba.*

(ix) *"Tutajenga zahanati." Wananchi walisema.*

(x) *Mwalimu alisema, "Kazi hii imenisaidia sana katika maisha yangu."*

E. Kuunda nomino za mahali kwa kutumia namba na herufi zilizomo katika jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni au kwenye bangokitita jedwali lililopo katika zoezi la 5 E ukurasa wa **162 - 163** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Tumia jedwali hilo kutoa mfano kwa kuunda jina la pekee Singida kwa kutumia mfano uliopo ukurasa wa **162** katika Kitabu cha Mwanafunzi.Tumia chaki au kalamu rashasha.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa **162 - 163** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) KILIMANJARO
(ii) DODOMA
(iii) KAGERA
(iv) ARUSHA
(v) MWANZA
(vi) MARA
(vii) GEITA
(viii) MBEYA
(ix) TABORA
(x) RUVUMA

F. Kupanga maneno katika sentensi ili zilete maana

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma sentensi kama zilivyo katika zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **163 - 164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 147 26/07/2021 12:02

(iii) Waeleze wanafunzi kuwa mpangilio wa maneno katika sentensi hizo hauleti maana.
(iv) Waongoze wanafunzi kupanga maneno katika sentensi kwa kutoa mifano. Anza na mfano uliopo katika zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **163** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(v) Toa mifano mingine ili wanafunzi waelewe zaidi.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 F lililopo ukurasa wa **163 - 164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Mdogo wangu anasoma shule ya awali.
(ii) Wakati wa likizo nitamtembelea bibi kijijini.
(iii) Kukopa harusi kulipa matanga.
(iv) Kila mwananchi hana budi kuufahamu wimbo wa taifa.
(v) Jana niliongea na mama kwa kutumia simu ya mkononi.
(vi) Mwalimu wetu anafundisha vizuri sana.
(vii) Kiswahili ni lugha ya taifa letu.
(viii) Sisi tulitembelea maktaba ya taifa.
(ix) Baraka amefaulu mtihani wake vizuri sana.
(x) Shule yetu imeshinda mashindano ya mpira wa miguu.

G. Kutunga sentensi kumi (10) sahihi kutokana na jedwali.

Hatua za ufundishaji

(i) Andika ubaoni au kwenye bangokitita jedwali lililopo zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(ii) Toa mifano kwa kuandika sentensi ubaoni au katika bangokitita kutokana na jedwali. Tumia mifano iliyopo kwenye zoezi hili.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 G lililopo ukurasa wa **164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 148 26/07/2021 12:02

H. Kuoanisha maneno ya safu A na maelezo yake katika safu B ili kuleta maana sahihi kwa kuandika herufi ya jibu kutoka safu B mbele ya neno la safu A

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu somo unalotaka kufundisha.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno ya safu A na maelezo ya safu B.

(iii) Tumia swali la kwanza kama mfano.

Mfano: *Jandoni - d*

(iv) Chagua mwanafunzi mmojammoja kuoanisha maneno ya safu A na maelezo yake kutoka safu B ili kuona kama wameelewa.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 H lililopo ukurasa wa **164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*d*	*(iv)*	*k*	*(vii)*	*g*	*(x)*	*e*
(ii)	*i*	*(v)*	*h*	*(viii)*	*j*	*(xi)*	*c*
(iii)	*a*	*(vi)*	*f*	*(ix)*	*b*		

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Ongoza majadiliano kuhusu rushwa na namna inavyoweza kutumika katika kumnyima mtu haki.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **164** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, usahihi wa sentensi na mtiririko wa mawazo.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 149 26/07/2021 12:02

Sura ya Kumi na Tisa

Kubaini hoja katika majadiliano

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza jinsi ya kubaini na kuchambua hoja kuu zilizotolewa kwenye mjadala. Vilevile, atajifunza msamiati, nahau, methali, uundaji wa maneno, mazoezi mbalimbali ya lugha na utungaji. Maarifa haya yatamsaidia kuwasiliana kwa Kiswahili fasaha katika miktadha mbalimbali.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma habari inayohusu **Urafiki wa mashaka**
(b) kubaini hoja katika majadiliano
(c) kuchambua hoja kuu katika majadiliano

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya methali, bangokitita, kalamu rashasha, chati ya nahau na chati ya alama za uandishi

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **165** katika Kitabu cha Mwanafunzi ili kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza.
(b) Ongoza mazungumzo mafupi kuhusu habari ya **Urafiki wa mashaka.**
(c) Ongoza majadiliano kwa kutumia picha iliyopo ukurasa wa **167** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(d) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Urafiki wa mashaka** iliyopo ukurasa wa **165 - 167** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kwa kidole na bila kutoa sauti.
(e) Waulize wanafunzi maswali yafuatayo:
    (i) Hivi unafikiri kwa nini hilo pori liliitwa Wachuki?
    (ii) Kwa nini Mama Digidigi aliingiwa na hofu?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 150 26/07/2021 12:02

(f) Waongoze wanafunzi kusimulia habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(g) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza la ufahamu lililopo ukurasa wa **168** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu habari itakayosomwa.
(b) Wakumbushe wanafunzi matumizi ya alama za uandishi kwa kuuliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili ili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia kanuni sahihi za usomaji.
(d) Waongoze wanafunzi kusoma mmojammoja kwa zamu bila kujali jinsi zao na viwango vyao vya usomaji. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, fuatilia usomaji wao ili ubaini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda ili kurekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Kazi ya kufanya (Igizo)

Hatua za ufundishaji

(a) Teua wahusika kwa kuzingatia wahusika waliopo kwenye hadithi.
(b) Toa maelekezo kwa wahusika.
(c) Wape muda wahusika kujiandaa na kuwasilisha kazi yao (igizo).
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **168** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Fanya hitimisho la igizo na wapongeze waliofanya vizuri.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 151 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Fundisha msamiati ufuatao: *jamii, dhuru, ng'ang'ania, majonzi, rarua, nduli, shuku, shari* na *kiongozi* kwa kutumia maelezo, matendo, mazingira halisi na picha.

(b) Andika maneno hayo ubaoni, na wanafunzi wayasome.

(c) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yanayofanana kwa kila neno walilopewa.

(d) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo kwa mazungumzo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(e) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi, kisha watunge sentensi nyingine kwa kuandika.

(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **168** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Wasirudie sentensi zilizotungwa wakati wa somo.

Somo la 5: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu kwa kutaja mianzo au miisho na wengine kukamilisha kisha kusema maana zake.

(b) Angalia usahihi wa miisho na mianzo ya methali walizozitaja wanafunzi.

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **168 - 169** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

1. *huvishwa pete*
2. *Mkono utoao*
3. *haubebi mtoto*
4. *Mtegemea cha nduguye*
5. *huonekana asubuhi*
6. *Mchunga ng'ombe*
7. *haishi kutapatapa*
8. *Akumulikaye mchana*
9. *Mkosa mafuta*
10. *uleule utaopoa*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 152 26/07/2021 12:02

Somo la 6: Nahau na misemo

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache kuonesha jinsi ya kutumia nahau na misemo katika sentensi. Mifano hiyo itokane na nahau na misemo iliyotumika katika hadithi yoyote waliyokwishaisoma katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Nakili ubaoni zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **169** katika Kitabu cha Mwanafunzi na waongoze wanafunzi kusoma nahau na misemo na maana zake. Waongoze kuanza kusoma sehemu A na baadaye sehemu B.

(iii) Tumia swali la kwanza kama mfano wa kuoanisha nahau na misemo na maana zake. Onesha namna ya kuandika majibu ubaoni.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **169** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*g*	*(v)*	*m*	*(viii)*	*k*	*(xi)*	*i*
(ii)	*f*	*(vi)*	*d*	*(ix)*	*b*	*(xii)*	*a*
(iii)	*e*	*(vii)*	*j*	*(x)*	*l*	*(xiii)*	*c*
(iv)	*h*						

Somo la 7: Mazoezi ya lugha

A. Kuunda maneno sahihi kumi (10) kwa njia ya kujirudiarudia

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache ya maneno yanayoundwa kwa njia ya kujirudiarudia (uradidi). Tumia mifano iliyopo zoezi la 6 A lililopo kwenye ukurasa wa **169** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 A lililopo ukurasa wa **169** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 153 26/07/2021 12:02

Majibu: *mbalimbali, vilevile, ileile, katikati, hapohapo, palepale, barabara, polepole, chapachapa, chepechepe (kumbuka majibu yatategemeana na majibu ya wanafunzi)*

B. Kutunga sentensi mbili kwa kila neno lenye maana tofauti

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayohusu maneno tata. Kumbuka maneno tata ni maneno yenye maana zaidi ya moja.

(ii) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yenye maana tata na kutunga sentensi kwa kutumia maneno haya. Tumia mfano uliopo katika zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa **169** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 B lililopo ukurasa wa **169 - 170** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

C. Kuandika sentensi kwa usahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusu makosa mbalimbali yanayoweza kutokea kwenye sentensi kama vile makosa ya tahajia, makosa ya kisarufi na makosa ya kimantiki.

- Wanyama wa porini amevamia kijiji chetu. Kosa la kisarufi
- Wanyama wa porini wamevamia kijiji chetu.

Kiambishi'wa' cha kwenye nomino kiendane na kiambishi'wa' cha kwenye kitenzi.

(ii) Toa mfano uliopo katika zoezi la 6 C ukurasa wa **170** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 C lililopo ukurasa wa **170** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 154 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) *Behewa la mizigo limedondoka.*
(ii) *Nywele zangu zimekuwa ndefu.*
(iii) *Wanafunzi wengi waliwahi kupata chanjo.*
(iv) *Nyota zimetanda anga lote.*
(v) *Macho yana kope.*
(vi) *Ndugu yangu unaitwa nani?*
(vii) *Funua ukurasa wa kitabu chako.*
(viii) *Sisi sote tufanye kazi kwa bidii.*
(ix) *Nta inanata sana.*
(x) *Fisi wanacheka msituni.*

D. Kupanga herufi ili kupata maneno sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Tumia mfano uliopo katika zoezi la 6 D ukurasa wa **170** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 D lililopo ukurasa wa **170** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *TANGAZO*
(ii) *HOJA*
(iii) *MAJADILIANO*
(iv) *HERUFI*
(v) *SOTE*
(vi) *THELATHINI*
(vii) *KISWAHILI*
(viii) *DIGIDIGI*
(ix) *MBOGO*
(x) *NYIKA*

E. Kubadili sentensi kuwa katika uyakinishi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayofafanua dhana ya uyakinishi.

(ii) Waongoze wanafunzi kubadili sentensi za ukanushi kuwa yakinishi. Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 6 E ukurasa wa **171** katika kitabu cha mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 E lililopo ukurasa wa **171** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 155 26/07/2021 12:02

F. Kupigia mstari viwakilishi katika sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mifano michache kwa kupigia mstari neno ambalo linawakilisha nafsi.

(ii) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 6 F lililopo ukurasa wa **171** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 F lililopo ukurasa wa **171** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Wao wanalima mazao yao ya biashara.
(ii) Nani atamfunga paka kengele?
(iii) Yeye anasumbua kula chakula.
(iv) Sisi tutafanya mitihani yetu ya kufunga shule wiki ijayo.
(v) Ninyi mtafyeka vichaka kuweka mazingira yote safi.
(vi) Wewe ndiye niliyekuwa nakutafuta.
(vii) Yule ni mchezaji hodari wa mpira wa miguu.
(viii) Mimi na yeye tunashirikiana katika masomo yetu.
(ix) Sisi na wao tutakwenda kutembelea mbuga za wanyama.
(x) Wale ni wauguzi waliokuja shuleni kwetu kutupatia chanjo ya homa ya manjano.

Somo la 8: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Ongoza mazungumzo kuhusu somo.

(b) Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mada ya utungaji kama ilivyobainishwa katika zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **171** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuwaongoza kwa kuuliza maswali yafuatayo:

(i) Utakwenda wapi wakati wa likizo?
(ii) Utafanya nini wakati wa likizo?

(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 7 lililopo ukurasa wa **171** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, uumbaji wa herufi, nafasi kati ya neno na neno, mtiririko mzuri wa mawazo, matumizi ya herufi kubwa na idadi ya maneno.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 156 26/07/2021 12:02

Sura ya Ishirini

Kusoma kwa ufasaha

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma habari kwa kuzingatia alama za uandishi. Pia, atajifunza mbinu za kusoma kwa usahihi na kwa kasi.

Shughuli za kutendwa na wanafunzi

(a) kusoma habari ya **Mafanikio ya Masaka** kwa ufasaha
(b) kuandika maneno yenye maana za jumla
(c) kutunga sentensi kwa kutumia maneno yenye maana za jumla katika mazungumzo
(d) kutunga habari kwa kuzingatia alama za uandishi

Mahitaji: vitabu, chati za maneno, kalamu rashasha, matini fupifupi, kadi za sentensi na picha (za kawaida na za mguso), bangokitita na diski (sidii za matini mbalimbali)

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yaliyopo ukurasa wa **172** kwenye kipengele cha *fikiri* katika kitabu cha Mwanafunzi.
(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya habari ya **Mafanikio ya Masaka** iliyopo ukurasa wa **172 - 174** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:
    (i) Je, umeshawahi kusoma habari yoyote?
    (ii) Je, uliona alama gani za uandishi?
(d) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **175** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 157 26/07/2021 12:02

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo. Eleza kile unachotaka kifanyike katika somo hili.

(b) Wakumbushe wanafunzi kuhusu matumizi ya alama za uandishi.

(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.

(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi na uwezo. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma.

(e) Baini dosari zinazojitokeza wakati wanafunzi wanasoma na uzirekebishe.

(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.

(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri inavyowezekana.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika ubaoni msamiati ufuatao: *vibarua, mrama, kiduchu, lukuki, nong'ona, viraka, gonga, mtaji, nawiri, wateja, shuhudia, shamiri, shahada, kampuni na kodi.*

(b) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno kwa mujibu wa habari. Unaweza kutumia mbinu ya maelezo, maswali na majibu, maigizo au mbinu nyingine.

(c) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo. Andika sentensi hizo ubaoni.

(d) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **175** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi watakazotunga hazifanani na zile zilizotolewa kwenye mifano.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 158 26/07/2021 12:02

Somo la 4: Miundo

Hatua za ufundishaji

(a) Waeleze wanafunzi jinsi ya kutumia miundo katika sentensi.
(b) Nakili ubaoni miundo yote iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **175 - 176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(c) Waongoze wanafunzi kuisoma miundo hiyo.
(d) Waelekeze wanafunzi kanuni za miundo hiyo.
(e) Tumia mifano iliyopo katika zoezi la 3 ukurasa wa **175 - 176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **175 - 176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 5: Mazoezi ya lugha

A. Kutunga sentensi kwa kutumia jedwali

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lililopo katika zoezi la 4 A ukurasa wa **176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyoko kwenye jedwali.
(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 A lililopo ukurasa wa **176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

B. Kuandika sentensi kwa kutumia alama sahihi za uandishi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayohusu matumizi sahihi ya alama za uandishi.
(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 B lililopo ukurasa wa **176** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 159 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) Mara nyingi, umaskini unatokana na kutokuwa na mpangilio mzuri wa kazi.
(ii) Juma aliweka akiba ya fedha na chakula kwa ajili ya maisha ya baadaye.
(iii) Mama yako anafanya kazi gani?
(iv) Kilimo cha matunda, nafaka na mbogamboga kina manufaa kwa jamii.
(v) Masaka alifanya biashara ya karanga, dagaa, vitumbua na magari.
(vi) Loo! Mbuzi ameanguka shimoni.
(vii) Baba yangu anaitwa Mashaka.
(viii) Mafanikio huanza kwa kutunza fedha kidogokidogo.
(ix) Mama anauza vitumbua. Baba anafanya kazi ya ulinzi./ Mama anauza vitumbua; baba anafanya kazi ya ulinzi./ Mama anauza vitumbua na baba anafanya kazi ya ulinzi.
(x) "Wewe unaitwa nani?" Kaka aliuliza.

C. Kuandika sentensi kwa usahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayohusu uandishi wa sentensi kwa usahihi.
(ii) Andika sentensi zilizokosewa ubaoni. Washirikishe wanafunzi kusoma sentensi hizo na kubaini makosa.
(iii) Ongoza wanafunzi kujadili makosa hayo na washirikishe kuyasahihisha.
(iv) Toa mifano mingine mbali na sentensi zilizoandikwa ubaoni kisha waongoze wanafunzi kuandika kwa usahihi katika madaftari.
(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 C lililopo ukurasa wa **176 - 177** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

*(i) Mtoto **alianguka** chini kwa kishindo.*
*(ii) Chuma kilichokatwa **kimeibwa** leo.*
*(iii) Jifunze biashara ukiwa na elimu **ya** msingi.*
*(iv) Dada **mkubwa** anacheza mpira vizuri.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 160 26/07/2021 12:02

*(v) Mwalimu Kilima anatufundisha **somo moja**.*

*(vi) Baba **yangu** ni mfugaji wa nyuki.*

*(vii) Kengele **iligongwa** saa sita mchana.*

*(viii) Nyaigera ni kitongoji ndani ya **Kijiji cha** Kemakorere.*

*(ix) Doto **ni** mkulima wa pamba.*

*(x) Viti **vilivyopangwa** vizuri **vimeanguka** chini.*

D. Kuandika neno moja linalobeba maana ya maneno yote kwa kila kifungu cha maneno

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo kuhusiana na somo linalofundishwa.

(ii) Toa mfano wa maneno na kuandika neno moja linalowakilisha kundi hilo.

Mfano: *parachichi, ndizi, chungwa, nanasi, embe (matunda)*
suruali, shati, sweta, gauni, koti (nguo/mavazi)

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 D lililopo ukurasa wa **177** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) vitafunwa (ii) vitoweo (iii) mikoa (iv) miezi (v) mbuga za wanyama (vi) nyumba/ majengo (vii) hewa/ gesi (viii) viungo vya chakula
(ix) wanyama/ reptilia (x) mapambo

E. Kuandika sentensi katika wakati ujao

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayohusu "wakati ujao."

(ii) Tumia mifano iliyopo zoezi la 4 E ukurasa wa **177** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iii) Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 E lililopo ukurasa wa **177 - 178** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 161 26/07/2021 12:02

Majibu:

(i) *Familia ya mzee Gibogo itaishi maisha ya dhiki.*
(ii) *Masaka ataridhika na hali ya maisha.*
(iii) *Mzee Gibogo ataishi kwa kufanya vibarua.*
(iv) *Mke wa mzee Gibogo atauza maandazi.*
(v) *Vijana watapaswa kuwa na fikira chanya kama Masaka.*
(vi) *Kaka yangu ataanzisha mradi wa kuuza karanga.*
(vii) *Mdogo wangu hatashindwa kwenda shuleni kwa sababu ya kukosa sare za shule.*
(viii) *Taifa litajengwa kwa kodi tutakazolipa.*
(ix) *Maisha yatabadilika kuwa mazuri sana.*
(x) *Masaka ataonesha uthubutu kwa kufanya biashara.*

F. Kubadili sentensi kuwa katika kauli ya kutendewa

Hatua za ufundishaji

(i) Toa maelezo yanayohusu kauli ya kutendewa. Kumbuka kauli ya kutendewa inajidhihirisha katika kitenzi kwa kuongeza herufi tamati **-iw-** , **-ew-** , **-liw-** , au **-lew-** baada ya mzizi wa kitenzi kabla ya irabu ya mwisho katika kitenzi.

(ii) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi. Washirikishe kuzibadili sentensi hizo katika kauli ya kutendewa.

(iii) Waongoze wanafunzi kujadili mifano iliyopo ukurasa wa **178** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

(iv) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 F lililopo ukurasa wa **178** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) *Shangazi amepasuliwa kuni zote zilizokuwa nje ya nyumba.*
(ii) *Mwanafunzi amesomewa kitabu cha Kiswahili.*
(iii) *Dada amepikiwa ugali laini sana.*
(iv) *Ng'ombe ameangushiwa mti uliokuwa pembeni mwa nyumba yetu.*
(v) *Mwanafunzi ametolewa darasani.*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 162 26/07/2021 12:02

(vi) Yahaya alichotewa maji ya kuoga.
(vii) Baba anapikiwa viazi kwa kutumia jiko la gesi.
(viii) Masaka anafugiwa kuku wa kienyeji kwa ajili ya kuuza.
(ix) Kijana atachezewa mpira vizuri.
(x) Msami ameandikiwa barua kwenda kwa rafiki yake.

G. Kusoma kifungu cha habari na kuweka alama za uandishi na herufi kubwa panapostahili

Hatua za ufundishaji

(i) Andika kifungu cha habari ubaoni kilicho na baadhi ya alama za uandishi.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma kifungu hicho. Baini makosa na kuyarekebisha.

(iii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 G lililopo ukurasa wa **178** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

Mimi ninaitwa Fikiri na baba yangu anaitwa Mawazo. Mimi na baba yangu tumejenga nyumba nzuri juu ya mlima mrefu. Tuliamua kufanya hivyo, baada ya kuvamiwa na wanyama wakali. Wanyama hao, walikuwa hatari kwa maisha yetu. Mwanzoni, baba alitoa wazo la kuhamia kijiji kingine. Baada ya kufikiri sana, nilimshauri baba tujenge nyumba juu ya mlima mrefu. Baba alikubali ushauri wangu.

Kazi ilianza na, hatimaye, nyumba ilikamilika. Nyumba ilikuwa imara sana. Ilijengwa kwa nondo, matofali, saruji, mbao na mawe. Juu ya mlima tulikojenga nyumba, wanatua ndege wa kila aina. Hatupati shida ya kitoweo. Ndege hao wanaingia ndani ya nyumba na tunawakamata kwa urahisi. Pia, miti ya matunda ya kila aina inapatikana juu ya mlima huo. Tunapata wageni wengi wanaokuja kununua matunda na nyama ya ndege.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 163 26/07/2021 12:02

Somo la 6: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo yanayohusu somo la utungaji.

(b) Waongoze wanafunzi kutambua mambo ya kuzingatia katika utungaji na uandishi wa kisa au habari.

(c) Wakumbushe wanafunzi kuzingatia maelekezo ya swali kama vile idadi ya maneno, kichwa cha habari, na mpangilio wa hoja.

(d) Wakumbushe wanafunzi kuhusu matumizi sahihi ya alama za uandishi. Waelekeze kuhusu matumizi sahihi ya herufi kubwa na ndogo. Wapatie mfano wa habari iliyotungwa.

(e) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 lililopo ukurasa wa **178** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 164 26/07/2021 12:02

Sura ya Ishirini na Moja

Kusoma kwa burudani

Utangulizi

Katika sura hii, mwanafunzi atajifunza kusoma kwa burudani **Kisa cha Mbuni na Mamba** kwa kuzingatia alama za uandishi. Vilevile, atajifunza msamiati, methali, vitendawili, mazoezi mbalimbali ya lugha, pamoja na utungaji.

Shughuli za kutendwa na mwanafunzi

(a) kusoma **Kisa cha Mbuni na Mamba** na kujibu maswali ya ufahamu

(b) kusoma kwa burudani **Kisa cha Mbuni na Mamba**

Mahitaji: vitu halisi, picha (za kawaida na za mguso), chati ya msamiati, kalamu rashasha na bangokitita

Somo la kwanza: Kusoma kimya

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kujibu swali lililopo katika kipengele cha *fikiri* ukurasa wa **179** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Lengo la maswali ya fikiri ni kukuza stadi ya kusikiliza, kuzungumza pamoja na kupata uelewa wa mwanzo alionao mwanafunzi kuhusu somo utakalofundisha.

(b) Waongoze wanafunzi kusoma kimya **Kisa cha Mbuni na Mamba** kilichopo ukurasa wa **179 - 181** katika Kitabu cha Mwanafunzi bila kufuatisha kidole wala kutoa sauti.

(c) Waongoze wanafunzi kujibu maswali yafuatayo:

(i) Mbuni alikuwa akipenda kwenda kunywa maji wapi?

(ii) Binadamu walikuwa wanamwinda nani ili wachukue ngozi yake?

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 165 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kujadili picha iliyopo ukurasa wa **180** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(e) Waongoze wanafunzi wasimulie habari waliyoisoma kwa maneno machache.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la kwanza lililopo ukurasa wa **181 - 182** katika Kitabu cha Mwanafunzi kwenye madaftari yao.

Somo la pili: Kusoma kwa sauti

Hatua za ufundishaji

(a) Toa maelezo mafupi kuhusu somo.
(b) Wakumbushe wanafunzi alama za uandishi kwa kuwauliza maswali.
(c) Soma aya moja au mbili kuonesha mfano mzuri wa usomaji sahihi kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, matamshi sahihi, kiimbo, kasi nzuri ya usomaji, matumizi sahihi ya alama za uandishi na kusoma kwa hisia.
(d) Waongoze wanafunzi mmojammoja kusoma kwa zamu, bila kujali jinsi zao na uwezo wao. Hakikisha wanafunzi wengi wanapata nafasi ya kusoma kadiri muda utakavyoruhusu.
(e) Wakati wanafunzi wanasoma, baini dosari zinazojitokeza na kuzisahihisha.
(f) Ukibaini makosa yanayojirudiarudia, sitisha usomaji kwa muda na rekebisha makosa hayo.
(g) Wanafunzi warudie kusoma kadiri wanavyopata nafasi.

Somo la 3: Msamiati

Hatua za ufundishaji

(a) Andika maneno yafuatayo ubaoni: *mamba, mbuni, chaka, okoa, angua, adui, sabahi, umiza, nasua* na *fukua,* kisha wanafunzi wayasome.
(b) Waongoze wanafunzi katika makundi wajadili maana za msamiati huo kwa kutumia vitu halisi, maelezo, vitendo, picha na maigizo.
(c) Waongoze wanafunzi kueleza maana ya msamiati kwenye zoezi la pili lililopo ukurasa wa **182** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 166 26/07/2021 12:02

(d) Waongoze wanafunzi kusoma msamiati na maana yake kwa kuzungumza.
(e) Angalia usahihi wa msamiati na maana zake.
(f) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la pili lililopo ukurasa wa **182** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha msamiati na maana zake ni sahihi.

Somo la 4: Methali

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutaja methali wanazozifahamu.
(b) Andika methali hizo ubaoni.
(c) Waongoze wanafunzi kutaja methali zinazotofautiana maana.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 lililopo ukurasa wa **182** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Somo la 5: Vitendawili

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kutega na kutegua vitendawili wanavyovifahamu.
(b) Wakumbushe wanafunzi namna ya kuanza na kuitikia kitendawili.

Mfano: kitendawili - *Tega*

Sijui aendako wala atokapo (upepo)
Akiondoka hawezi kurudi (jani la mti)

Endapo mwanafunzi hatatoa jibu sahihi, mtegaji apewe mji ili atoe jibu sahihi.

(c) Waongoze wanafunzi kwa kutumia maelezo, picha na mifano kutega na kutegua vitendawili.
(d) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 lililopo ukurasa wa **182 - 183** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 167 26/07/2021 12:02

Majibu:

1.	*kinyonga*	*6.*	*mafiga*
2.	*kinu*	*7.*	*tonge liendalo mdomoni*
3.	*ng'ombe*	*8.*	*mvua*
4.	*mbwa*	*9.*	*tetea akiatamia mayai*
5.	*kucha*	*10.*	*mvi*

Somo la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kuchagua jibu sahihi ili kumalizia sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Toa mfano kwa kuandika swali ubaoni ili wanafunzi wachague jibu lililo sahihi.

Mfano: Ngozi ya mamba hutumika kutengenezea *viatu, mikanda* na *mikoba*.

(a) viatu, mikanda na mikoba
(b) viatu, mikanda na meza
(c) mikanda sahani na viatu
(d) mapambo, viatu na nguo

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 A lililopo ukurasa wa **183 - 184** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i)	*a*	*(iv)*	*c*	*(vii)*	*c*	*(ix)*	*b*
(ii)	*a*	*(v)*	*d*	*(viii)*	*a*	*(x)*	*a*
(iii)	*b*	*(vi)*	*b*				

B. Kuchagua neno moja kutoka kila safu ili kuunda sentensi sahihi

Hatua za ufundishaji

(i) Nakili ubaoni jedwali lenye safu A, B na C likiwa na maneno yake.

(ii) Waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo kwa sauti.

(iii) Waongoze wanafunzi kutaja maneno yaliyoko kwenye safu zote yanayoendana.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 168 26/07/2021 12:02

(iv) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia maneno hayo.
(v) Andika sentensi hizo ubaoni.
(vi) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 B lililopo ukurasa wa **184** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(vii) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia usahihi wa sentensi, alama za uandishi, herufi kubwa na mwandiko safi.

Majibu:

(i) Mbuni anaishi porini.
(ii) Mbuni anaatamia mayai.
(iii) Mamba anaishi mtoni.
(iv) Maji yamefurika mtoni.
(v) Jogoo huwika alfajiri.
(vi) Bata anaatamia mayai.

C. Kukanusha sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mfano uliopo zoezi la 5 C ukurasa wa **185** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuongeza mifano mingine.
(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 C lililopo ukurasa wa **185** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) Juma hakusoma kitabu cha hadithi ya sungura.
(ii) Mimi sitaenda tena mtoni kuteka maji.
(iii) Wanafunzi hawakucheza mpira na kufunga magoli mengi.
(iv) Leo hakuna upepo mkali sana.
(v) Wazazi wa Agata hawakulima mashamba makubwa.
(vi) Mtoto hajavaa nguo zinazong'aa.
(vii) Mfuniko wa pipa lililonunuliwa jana, haujatoboka.
(viii) Dada yangu hajui kuoka mikate mizuri sana.
(ix) Wananchi hawajajiwekea utaratibu wa kufyeka nyasi pembezoni mwa barabara.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 169 26/07/2021 12:02

(x) Mariamu hajaosha vyombo vyote vilivyotumika wakati wa sherehe.

D. Kuandika maana mbili kwa kila neno na kutunga sentensi

Hatua za ufundishaji

(i) Andika maneno yenye maana zaidi ya moja ubaoni, kisha waongoze wanafunzi kusoma maneno hayo kwa sauti.

(ii) Fundisha maana za maneno kwa kutumia mfano mmojawapo.

Mfano: *1. ua - sehemu ya mmea*

2. ua - wigo unaojengwa kuzunguka nyumba

(iii) Waongoze wanafunzi kueleza maana za maneno yaliyoandikwa ubaoni.

(iv) Waongoze wanafunzi kutunga sentensi mbili kwa kutumia mojawapo ya maneno hayo. Angalia usahihi wa sentensi walizotunga wanafunzi.

Mfano: *Ua hili linanukia vizuri sana.*

Baba amejenga ua kuzunguka nyumba yetu.

(v) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 D lililopo ukurasa wa **185** katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha sentensi zilizotungwa ni sahihi ili kuondoa utata wa neno.

Majibu:

Maana za maneno

(i) **poa**
- *pungua joto*
- *kitendo cha mtu kukaa kimya kwa utulivu bila vurugu yoyote*

(ii) **mto**
- *mtiririko asilia wa maji kuelekea baharini au ziwani*
- *mfuko uliojazwa manyoya au sufi unaotumika kuegemeza kichwa aghalabu wakati wa kulala*

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 170 26/07/2021 12:02

(iii) **mbuni**
- *mmea wa asili ya miti unaotoa maua na kuzaa matunda yaitwayo kahawa*
- *ndege ambaye ni mkubwa mwenye miguu mirefu anayekimbia kwa kasi bila ya kuruka*

(iv) **kibao**
- *pigo kwa kutumia kiganja*
- *kikalio*

(v) **angua**
- *angusha matunda kutoka mtini kwa kutumia mikono au kipande cha mti*
- *fanya kinda au kifaranga kitoke chenyewe katika yai la ndege*
- *toa sauti ya juu ambayo aghalabu huashiria kuomba msaada au kuonesha furaha*

(vi) **lia**
- *toa machozi au sauti kutokana na maombolezo au majonzi*
- *toa sauti kama vile kengele, mnyama, risasi au redio*

(vii) **kucha**
- *muda wote kabla ya kupambazuka*
- *kipande kigumu katika vidole vya miguu na mikono ya binadamu, mamalia na ndege ambacho hukuna na kufunika sehemu ya juu ya kidole*

(viii) **hema**
- *kibanda kilichotengezwa kwa turubai*
- *kitendo cha kutoa pumzi kwa nguvu kutokana na kazi fulani*

(ix) **washa**
- *hali ya kuchonyota kwa mwili inayomfanya mtu ajikune*
- *sababisha moto uwake kwa kupekecha au kutumia kiberiti*

(x) **kuna**
- *kuwepo kwa kitu au mtu fulani katika mazingira maalumu*
- *kwaruza au kwangua kwa kucha*

E. Kuoanisha sehemu A na sehemu B ili kukamilisha maelezo ya sehemu A

Hatua za ufundishaji

(i) Waongoze wanafunzi kwa kutumia mifano ya maneno yaliyopo katika sehemu A na maelezo yake katika sehemu B.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 171 26/07/2021 12:02

Mfano:

Sehemu A	Sehemu B
(i) Hutokea ghafla na kusambaa kama moshi_____	ukungu

Katika mfano huo, maneno *hutokea ghafla na kusambaa kama moshi* linaendana na neno *ukungu* ambalo limeoneshwa katika safu ya maelezo ya sehemu B.

(ii) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 E lililopo ukurasa wa **186** katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Majibu:

(i) ukungu
(ii) baridi
(iii) ukame
(iv) kimbunga
(v) unyevu
(vi) ngurumo
(vii) mvua
(viii) wingu
(ix) joto
(x) mafuriko

Somo la 7: Utungaji

Hatua za ufundishaji

(a) Waongoze wanafunzi kupendekeza kichwa cha habari kinachohusu wanyama ambacho wanafunzi wataandika habari juu yake.
(b) Waongoze wanafunzi kutaja mambo ya kuzingatia katika uandishi wa kisa cha wanyama. Kama vile sifa za wanyama hao na tabia zao.
(c) Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la 6 lililopo ukurasa wa **186** katika Kitabu cha Mwanafunzi.
(d) Sahihisha kazi za wanafunzi kwa kuzingatia alama za uandishi, mwandiko, mtiririko wa mawazo, nafasi kati ya neno na neno, uumbaji wa herufi, matumizi ya herufi kubwa, idadi ya maneno pamoja na mantiki ya kisa chenyewe.

KIONGOZI DARASA LA 6_KIONGOZI_CORRECTIONS.indd 172 26/07/2021 12:02